**MWINYI** abainisha mgomo wa walimu ulivyotikisa serikali

UKURASA 3



**MWANAFUNZI** aliyedaiwa kumtoroka sista kanisani akutwa amejinyonga

UKURASA 4



ama

ALHAMISI MEI 20, 2021 AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 12

MAMBO YA JKCI...
Prof. Janabi: Haya ndio mapinduzi namna tunavyotibu umeme moyo

Ukurasa 14

MAGEUZI YA DEMOGRAFIA
Kudhibiti uzazi China kunavyomaliza idadi vijana, watoto, nguvukazi taifa

**Wanaharakati walivyoamka na yao kujadili bajeti ya Waziri Gwajima**

Na Yasmine Protace

AFYA ni nini? Jibu la jumla linaangukia katika tafsiri ya jumla kwamba, ni maisha ya kila siku yanayohusisha mwili wa mtu, ikianza na nyenzo kama moyo, ubongo, viungo vingine na mazingira yanayomzunguka.

Hapo mtu kila akifanyacho, inabeba tafsiri katika maisha yake. Ni namna gani anahusika au kutohusika nayo, inakuja na tafsiri ya ama kumjenga au kumbomoa kimaisha kwa kuangukia tafsiri ya afya.

Namna afya hiyo na vigezo vyake vinahudumiwa hata kuleta sura ya matokeo, iwe chanya au hasi, hutegemea tofauti kati ya mtu mmoja na mwingine, katika uelewa wake, anavyochukulia uzito na tafsiri kulingana na tofauti kati yao.

Hivyo, jamii inatakiwa kuzingatia masuala ya afya kuepukana na kupata magonjwa ya aina yoyote, jambo ambalo nchini serikali kupitia Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, ina hatua inazochukua kufanikisha mtazamo huo.

Mojawapo inayojulikana ni haja ya kuwapo bima ya afya inayomfikia kila mtu nchini, ambayo waziri mwenye dhamana, Dk. Dorothy Gwajima, katika mapendekezo ya mapato na matumizi ya mwaka ujao wa fedha, ana orodha ya namna yaliyoandaliwa kuboreshwa kwa ajili ya kuingizwa katika upatikanaji bima.

Ofisa Programu kutoka TGNP Mtandao, Anna Sangai. **PICHA: MTANDAO**

**MAONI YA WADAU**

Baada ya kuwasilishwa makadirio hayo ya mapato na matumizi hivi karibuni, wadau wa Semina za Jinsia na Maendeleo GDSS zinazofanyika jijini Dar es Salaam, nao waliwasilisha mapendekezo, wakiwa na mitazamo kadhaa.

Janeth John, mshiriki wa GDSS anakiri kusikia maelezo ya makadirio ya mapato na matumizi, akiwa na ufafanuzi: "Inatakiwa elimu ya ukatili ianze kutolewa shule ya msingi na kuendelea ili watoto wanapofanyiwa ukatili waweze kutoa taarifa."

Janeth anasisitiza umuhimu wa nyumba za ibada na mikusanyiko ya watu kama makundi ya vikoba kutolewe elimu stahiki, kuoanisha mahitaji ya kiusalama kwa umma.

Mshiriki huyo anasema, uboreshaji wa miundombinu katika hospitali na vituo vya afya unapaswa kuangalia namna baadhi ya maeneo na hasa vijijini, ambako miundombinu yake haikidhi mahitaji ya umma na kusababisha malalamiko mengi ya jamii.

Ofisa Programu kutoka TGNP Mtandao, Anna Sangai, anasema asasi yake inayotumia utetezi wa haki za kijinsia na watoto, anaeleza wanavyovutiwa na maboresho makubwa ambayo wizara yenye dhamana na afya, imeshajipanga kuyafanya.

Anasema katika miundombinu, suala la kufunguliwa vituo vya afya pasipo kukamilika kwa miundombinu na mahitaji muhimu katika uendeshaji wake, ni jambo linalochangia malalamiko kutoka kwa umma wa walengwa.

"Tusikimbilie kufungua vituo vya afya, kama vinakuwa bado inabidi kusubiri vikamilike, ili viweze kutoa huduma zilizo sahihi," anafafanua, Anna, msomi mwandamzi katika stadi za ualimu na taaluma ya maendeleo.

Mdau mwingine, Nyajura Kakinde, anasema kutolewa mikopo kwa wanawake ni jambo jema, lakini ana angalizo katika umuhimu wa usimamizi wake sahihi.

Ana ushauri kwamba, kinamama wanapaswa wasimamiwe vyema katika mwenendo wao wa kijamii na kiuchumi, hata wafanikishwe kupata pesa zitakazowakomboa kimaisha.

Mshiriki wa mjadala kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Veronica Meaipole, anataja haja ya bima ya kila mtu ni njema, lakini ikiwa na maelezo ya kina kuhusu matibabu husika yatakavyotolewa.

UKURASA 11


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Alhamisi Mei 20, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580586

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


# LUKU YAPONZA VIGOGO

## **WABUNGE** waibana serikali, waziri atinga TANESCO... *Endelea Ukurasa 3*




Sehemu ya msururu wa wananchi katika ofisi ya Shirika la Umeme nchini (TANESCO) Magomeni, mkoani Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kununua Luku, baada ya huduma hiyo kuwa na hitilafu kwa siku ya tatu sasa na kusababisha usumbufu mkubwa kwa watumiaji. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## CHADEMA YACHAGUA WARITHI WA KINA MDEE

UKURASA 4

## Ma-RC waonywa kujigeuza miungu watu, ulevi na uzinzi

UKURASA 2


**MICHEZO** AMA ZAO AMA ZETU UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6




Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Makamu wa Rais Dk. Philip Isdor Mpango, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Hamis Juma, Spika wa Bunge Job Ndugai, Katibu Mkuu (Ikulu) Dk. Moses Kusiluka pamoja na wakuu wapya wa mikoa, baada ya kuwaapisha Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## ...abadili 'gia angani'

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amefanya mabadiliko ya wakuu wa mikoa wawili muda mfupi baada ya kuwaapisha Ikulu jijini Dar es Salaam jana huku sababu kubwa ikiwa ni uzoefu.

Baada ya kuwaapisha wakuu wa mikoa 10 kati ya 26 na wakuu wa taasisi mbalimbali aliowateua mwishoni mwa wiki iliyopita, Rais Samia alitangaza kumhamisha David Kafulila katika Mkoa wa Arusha aliopangiwa awali kwenda kuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu.

Alisema Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, John Mongella, anakwenda kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha kwa sababu alikuwa anaongoza mkoa mkubwa ambao ulikuwa unaendelea kuwa Jiji na Arusha ni Jiji.

"Na Kafulila kwa sababu ndiyo anaanza, alikuwa RAS (Katibu Tawala Mkoa) na anaanza kuwa Mkuu wa Mkoa, utakwenda Simiyu, nimefanya mabadiliko haya, maelekezo mengine tutapeana ndani ya kikao cha ndani," alisema.

Aliwapongeza walioteuliwa na kuapa na kuwaeleza kuwa Tanzania inakaribia watu milioni 60 na asilimia 15 wangefaa kuteuliwa katika nafasi hizo, lakini Mungu ameelekeza wateuliwa wao.

Baada ya hafla hiyo, Rais Samia alifanya kikao cha kazi na wateule hao.

# Ma-RC waonywa ulevi, uzinzi

**Na Romana Mallya**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai wamewafunda wakuu wa mikoa na wilaya, wakiwataka kutojivika cheo cha Rais maeneo yao, kutoonea watu, kuacha migogoro, ulevi na uzinzi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana Ikulu jijini Dar es Salaam wakati wa kuapishwa kwa wakuu wa mikoa na viongozi wa taasisi mbalimbali walioteuliwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan, viongozi hao pia waliwataka wakachape kazi, kukusanya mapato na kutatua matatizo ya wananchi.

Spika Ndugai alisema wapo wakuu wa wilaya na mikoa, huko nyuma waliamini kule walipo ni Rais wa Mkoa au Rais wa Wilaya.

"Utasikia mimi ni Rais wa Mkoa huu au Rais wa Wilaya hii, nani amesema? Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Rais ni Samia Suluhu Hassan basi, huo ndiyo ukweli, msije mkajidanganya kwamba wewe ni Rais, ndiyo maana tunapotunga sheria tunaandika Rais ata... hatuandiki Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunaandika neno moja 'Rais' kwa sababu Rais ni mmoja.

"Mnajivisha koti siyo lako matokeo yake unaweza kufanya mambo ambayo ukidhania wewe ni Rais," alionya.

**TAKUKURU IACHE UONEVU**

Spika Ndugai pia alimtaka Mkurugenzi Mkuu wa Taaasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Kamishna wa Polisi Salum Hamduni kushughulikia alichokiita uonevu.

"Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, atafikisha ujumbe wetu unaohusu uonevu mkubwa unaofanywa na TAKUKURU, mjiangalie upya, siyo vizuri kuonea watu, haipendezi hata kidogo," alisema.

Spika Ndugai pia alimpongeza aliyekuwa Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai, kwa utendaji wake bungeni. Kagaigai sasa ni Mkuu wa Mkoa.

"Lakini, Rais umetupatia Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi, ambaye anaingia katika rekodi za nchi kuwa mwanamke wa kwanza toka Uhuru kuwa Katibu wa Bunge la Tanzania," alisema.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisema hatarajii viongozi waliopewa nafasi kuwa mfano mbaya, hawachapi kazi na kuwa na tabia zisizofaa.

"Sitarajii walevi kati yenu, sitarajii orodha ya wazinzi itakayofika kwetu kutoka kwenu, na mengine maovu katika jamii.

"Moja wa wajibu wa viongozi hasa Wakuu wa Mikoa, ukiacha kuhakikisha amani na usalama, ni muhimu kujua kwamba kazi kubwa ni kusimamia uchumi wa mkoa, kuongeza uzalishaji katika kilimo na viwanda na kusimamia tija na kuangalia masoko ya wananchi," alisema.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliwataka viongozi hao watambue majukumu ya nafasi walizonazo na mipaka ili wafanye kazi vizuri.

Alisema matarajio yao, watashirikiana ili kujua nini kinatakiwa kufanyika na kutatua matatizo ya wananchi na kuhakikisha maeneo yao yanabaki kuwa salama.

# Jaji Mkuu: Kesi 310 zimevuka muda Kisutu

**Na Romana Mallya**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amekiri kuwapo kwa ucheleweshaji wa kesi mahakamani, akibainisha kuwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu pekee, hadi jana kulikuwa na kesi 310 zilizovuka muda wake.

Akizungumza jana Ikulu jijini Dar es Salaam wakati wa kuapishwa kwa wakuu wa mikoa, wakuu wa taasisi walioteuliwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan, alisema mahakamani wanasema kesi hizo zinaingia katika eneo la mrundikano.

Kutokana na tatizo hilo, Jaji Mkuu Juma amewataka wateule wapya, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Kamishna wa Polisi Salum Hamduni, kutembelea tovuti ya mahakama ili wajipange katika kurekebisha.

Alisema mahakama kupitia tovuti yake huweka takwimu za maeneo gani yenye ucheleweshaji mkubwa wa kesi kwa sababu wameweka utaratibu zikifikia muda fulani katika mtandao huo zinaonyesha rangi nyekundu.

"Leo (jana) nimepitia tovuti ile, kuangalia ni kesi gani ambazo zimecheleweshwa ambazo zinaonyesha rangi nyekundu, nimekuta katika Mahakama ya Kisutu kuna kesi kama 310 ambazo zimevuka muda ambao mahakamani tunasema zinaingia katika eneo la mrundikano," alisema.

Pia amewaomba wakuu hao wa taasisi hizo mbili zilizovaa viatu vya utoaji haki, kuangalia kama upo upungufu wa utoaji sheria na kuwa mstari wa mbele kuutatua.

"Ninawaomba kitu cha kwanza msione haya kubadilisha sheria kwa sababu zimetungwa katika zama ambazo ni za zamani kidogo na tupo katika zama ambazo wananchi wanataka haki kwa haraka zaidi," alisema.

Alisema DDP na Mkurugenzi Mkuu TAKUKURU ni wadau muhimu wa mahakama kwa sababu mnyororo wa haki unaanzia kwenye ngazi ya upelelezi na huishia mahakamani.

"Ndiyo maana tunaambiwa haki ya mwisho utaipata mahakamani, lakini mwanzo wa haki utaipata wakati wa upelelezi, wakati wa kuendesha kesi na vilevile wakati ikiendelea mahakamani.

"Kwa nafasi ya DPP, huyu ni mtu muhimu katika mfumo wa utoaji haki, amepewa hadhi ya kipekee na katiba, kabla ya 2005, DPP alitajwa katika sheria ya kawaida, lakini mabadiliko ya katiba yakapandisha hadhi na kuwa sehemu ya katiba na ana kazi tatu.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Zanzibar, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Massoud Ali Mohammed, akizungumza na wakuu wa vikosi vya idara maalum za SMZ, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar jana, baada ya kupitishwa kwa makadirio na matumizi ya bajeti ya wizara yake. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi asema mgomo wa walimu ulimtikisa

**Na Enock Charles**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amesema kipindi cha pili cha uongozi wake (1990-1995) kiligubikwa na migomo mikubwa ya wafanyakazi ukiwamo wa walimu, anaokiri ulimkera na kumuudhi.

Katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anabainisha jinsi alivyokerwa na mgomo huo kiasi cha kulazimika kuwasimamisha kazi baadhi ya watumishi hao.

Anasema Chama cha Walimu Tanzania kilichoanzishwa mwaka 1993 ndicho kilichoasisi mgomo huo baada ya kumwandikia barua ya kutaka aonane na walimu wote wa Dar es Salaam, kipindi hicho kukiwa na walimu wapatao 4,000.

Anasema walimu hao walikuwa na malalamiko yao yaliyohusu posho na stahiki zao mbalimbali wakati huo yeye akiwa nje ya nchi.

"Lakini barua yao ilifika Ikulu wakati nipo safarini nje ya nchi. Na enzi zile mawasiliano hayakuwa kama ilivyo leo ambapo upo wepesi wa kusafirisha nyaraka kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

"Kwa vile sikuwapo nchini sikuwahi kuisoma na kuijibu barua yao. Walipoona kimya, wakaamua kuwa nimewapuuza na wakaitisha mgomo, hata kabla sijarejea nchini," anasimulia.

Anasema baada ya kurejea nchini na kukuta walimu hao tayari wameitisha mgomo wa nchi nzima, aliamua kuwaita viongozi wao kwenda Ikulu kumuona.

"Najua walimu mlitaka kuniona kwa muda kidogo na leo siku ya kuniona imefika. Karibuni Ikulu. Karibuni nyumbani kwenu. Niko tayari kusikiliza matatizo yenu, malalamiko yenu, rai yenu na maoni yenu juu ya kazi zenu, na kuhusu maslahi yenu. Uwanja uko kwenu. Karibuni," anakumbusha alivyowakaribisha Ikulu.

Anasema Mwenyekiti wao, Peter Mashanga, kipindi hicho mwalimu wa Shule ya Azania na Katibu wa Chama cha Wafanyakazi (OTTU) tawi la shule hiyo, alimwambia walikwenda pale kupokea waliyomwandikia katika barua, jambo lililoonyesha hawakuwa tayari kwa majadiliano isipokuwa kupewa kile walichokitaka.

Mwinyi anasimulia kuwa baada ya kusikiliza hoja za walimu, alibaini walisukumwa na wanasiasa katika kudai maslahi makubwa kupita kiasi ambayo yalikuwa hayatekelezeki kwa viwango vya kiuchumi vya serikali ya wakati ule na ndiyo sababu awali walimtaka akutane na walimu wote 4,000 wa Dar es Salaam ili wamtishe kwa wingi wao.

Walimu hao walidai kila mwalimu kwa mwezi alipwe Sh. 60,000 kwa ajili ya posho ya chakula, Sh. 60,000 posho ya usafiri, Sh. 60,000 posho ya nyumba na Sh. 60,000 posho ya matibabu.

"Wakati ule Dola moja ya Marekani ilikuwa sawa na Sh. 450 hivyo kwa viwango vya posho hizo nne jumla yake ikiwa Sh. 240,000 ingelikuwa ni sawa na Sh. 1,190,000 kwa viwango vya sasa," anafafanua.

Mwinyi anasema walimu hao pia walitaka viwango vipya vya mishahara na marupurupu vinavyoanzia Sh. 524,000 hadi 1,020,000 za wakati ule na anasema walipofanya mahesabu ya madai hayo, ilikuwa ni sawa na fedha za matumizi ya serikali nzima kwa miaka mitatu.

Anasema madai hayo hayakuwa madai halali bali aliyaona ni yenye lengo la kutafuta kisa cha kupambana na chama tawala na serikali yake kwa msukumo wa wanasiasa, jambo ambalo lilimkera.

Hata hivyo, Mwinyi anakiri yalikuwapo baadhi ya madai halali ya walimu hao kama vile suala la kukawia kupata mishahara yao, akiwageukia viongozi wa Wizara ya Elimu akiwamo Waziri na Katibu Mkuu wake na kuwaambia hilo lilikuwa kosa kwao na kuwaahidi walimu kulipwa mishahara wakati uleule wanapolipwa watumishi wengine.

# Luku yawaponza vigogo TANESCO

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amewasimamisha kazi maofisa watatu wa Shirika la Umeme (TANESCO) kwa siku 10 kwa kushindwa kutatua tatizo la mfumo wa Luku.

Dk. Kalemani alizuru ofisi za shirika hilo na kumwagiza Mkurugenzi Mkuu kuhakikisha ifikapo saa nane mchana jana, mfumo huo uwe umerejea.

"Mnaleta maneno ya mchakato, wasimame siku 10 wakichunguzwa, wakionekana hawana hatia mtawarejesha, wana hatia mwisho, huyu na ma-principal wawili, ninataka kuona leo (jana) maelezo yako, ikifika saa 10 jioni niyapate kama unafaa kwenye nafasi yako," alisema huku akiagiza wateuliwe watu wengine wa kuendesha mfumo huo wakati hao wakiwa wamesimama.

Dk. Kalemani alielekeza mfumo huo uendeshwe na Watanzania na hataki kusikia una uhusiano na nje tena baada ya kumaliza kwa mkataba uliopo, Januari mwakani.

Taarifa ya TANESCO jana ilielekeza wateja kununua umeme katika ofisi zake za mikoa na wilaya wakati wataalamu wakiendelea na kazi ya utatuzi wa ununuzi kupitia njia za kielektroniki.

**BUNGENI**

Jijini Dodoma jana wabunge waliibana serikali bungeni kuhusu suala hilo, Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, akikiri kuwapo kwa tatizo hilo.

Mbunge wa Mafinga Mjini (CCM), Cosato Chumi, alisema amepokea simu nyingi na ujumbe kutoka kwa wananchi wakisema wanashindwa kulipia huduma ya umeme kwa siku ya pili jana. Byabato alikiri kuwa kwa siku tatu kuna tatizo hilo na linatokana na mfumo huo na kumhakikishia kuwa suala hilo lilikuwa linashughulikiwa.

"Tuna mifumo miwili mfumo mmoja umekufa umepata hitilafu kidogo na umepelekwa kutengenezwa na iliyobaki inabeba mzigo mkubwa sana inashindwa kuhudumia wateja wote kwa wakati," alisema.

●**Imeandikwa na Romana Mallya (DAR) na Augusta Njoji (DODOMA)**



# Wapya waziba nafasi za kina Mdee BAWACHA

**Richard Makore na Neema Emmanuel,** MWANZA

BARAZA la Wanawake la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), limehitimisha kikao chake jijini Mwanza kwa kumchagua Catherine Ruge kuwa Katibu Mkuu wa baraza hilo.

Uchaguzi huo umekuja baada ya aliyekuwa anashikilia nafasi hiyo, Grace Tendega, kuvuliwa uanachama wa chama jicho kwa madai ya kuwa miongoni mwa wasaliti kwa kukubali uteuzi wa ubunge viti maalum.

Aidha, Sharifa Seleman amepewa nafasi ya kukaimu uenyekiti wa baraza hilo, baada ya aliyekuwa anashikilia kitu hicho, Halina Mdee naye kuvuliwa uanachama na wenzake 18.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo juzi usiku, msimamizi wa uchaguzi huo, Ruth Molell, alisema Catherine akipata ushindi wa asilimia 52.

Alisema nafasi hiyo ilishindaniwa na wagombea watatu ambao ni pamoja na Asia Msangi aliyepata kura 8, Ester Dafi kura 23 na mshindi akajinyakulia kura 34.

Nafasi ya Naibu Mkuu Zanzibar ilinyakuliwa na Bahati Chumu Haji akipata kura za ndiyo 60 sawa na asilimia 92.3 na za hapana kura tano. Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Bara Nuru Ndossi aliibuka mshindi kwa kujinyakuliwa kura 33 na kuwabwaga Blends Rupia aliyepata kura 17 na Emma Boki kura 15.

Nafasi nyingine iliyopigiwa kura ni Mratibu wa Uenezi wa Baraza hilo, Aisha Ame akipata kura 36, na kumshinda, Husna Said (kura 23).

Akizungumzia baada ya kutangazwa mshindi, Catherine aliahidi ushirikiano na wanawake wote wa baraza hilo pamoja na kusimamia mipango yote waliyojiwekea.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisisitiza umuhimu wa katiba mpya ili kusimamia uchumi pamoja na kuleta maendeleo ya nchi.

Alitoa kauli hiyo wakati wa ufunguzi wa kikao cha BAWACHA jijini Mwanza kwa ajili ya kufanya uchaguzi wa nafasi zilizoachwa wazi baada ya viongozi waliokuwapo kufukuzwa uanachama.

Kikao hicho cha kamati tendaji ya BAWACHA kilikuwa na ajenda moja ya kufanya uchaguzi wa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Bara, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar na Mratibu wa Uenezi.

Alisema BAWACHA wana kazi ya kuwatetea wanawake na kuhamasisha upatikanaji wa katiba mpya, ili kusimamia uchumi wa nchi na maendeleo.

Aliongeza kuwa jukumu lingine la wanawake wa CHADEMA linalotokana na sera yao ni kusimamia mustakabali wa wanawake kabla na baada ya kuingia madarakani kwenye uchumi, huduma za kijamii na mambo yote ya haki za msingi.

Aliongeza kuwa katiba mpya itasaidia kutengeneza usawa, haki na fursa kwa wote na kwamba wanawake wa chama hicho kuhakikisha taifa linakuwa na jamii yenye usawa na haki katika kusimamia masuala ya kijinsia.

Alisema uchaguzi huo umefanyika kwa mujibu wa Katiba yao ibara ya 7.85 kwa mamlaka ya kamati ya utendaji wa baraza hilo.

Mnyika alisema kupitia baraza hilo wana nafasi pekee ya kuandika historia kwa sababu wale ambao walikuwa nao katika mapito magumu ya uchaguzi mwaka 2020, baada ya uchaguzi kumalizika waliona ni afadhari wasaliti,

"Ni lazima katikati ya usaliti, uasi na ubinafsi wengine wasonge mbele kwa kuweka pembeni ubinafsi na kuwe na haki, kinamama mhakikishe mnakuwa mstari wa mbele wa kuhakikisha taifa linakuwa na tume huru ya uchaguzi na viongozi mnapaswa kulisimamia jambo hili, mnajua miongoni mwenu wengi katika uchaguzi wa mwaka 2020 mlisimamisha kinamama zaidi ya 60 kwenye majimbo," alisema Mnyika.

Akizungumzia nafasi ya mwenyekiti wa BAWACHA taifa, Mnyika alisema kamati tendaji imemteua Sharifa Suleiman ambaye ni makamu mwenyekiti kukaimu nafasi hiyo hadi hapo watakapofanya uchaguzi.

Kwa upande, Sharifa aliwataka viongozi waliochaguliwa kuwa na hekima katika mwenendo wa kufanya maamuzi yatakayokuwa na adhima ya kulivusha baraza hilo na kuwa imara.

Alisema katika chama hicho uongozi siyo utumishi bali ni uwajibikaji ulio imara usio tayari kufanya maamuzi yasiyosahihi na wachague viongozi wasiofanya makosa kama yaliyotokea.

"Hakuna mtu yeyote aliye juu ya mwenzake, kuna watu wanajiona bora kuliko watu wengine msije mkafanya makosa kinachotakiwa ni kupata viongozi bora na siyo bora kiongozi," alieleza Sharifa.

Aliongeza kuwa baada ya mkutano huo BAWACHA imejipanga kufanya ziara mikoa yote ili kuhakikisha baraza linakuwa bora kuliko nyakati zilizopita na kutoa fursa ya kuwaandaa wanawake na kuwajengea uwezo wa kushiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi kipindi cha uchaguzi ujao.



Fundi mizani, Kailan Hussein akirekebisha mzani wa hospitali ya Vijibweni Kigamboni, mkoani Dar es Salaam, wakati Wakala wa Vipimo (WMA), walipotembelea kuhakiki mizani zinazotumika hospitalini hapo jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mwanafunzi aliyedaiwa kumtoroka Sista kanisani akutwa amejinyonga

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MWANAFUNZI wa kidato cha tano katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Peramiho katika Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, Sophia Joel Mbano (19), amekutwa amekufa, baada ya kujinyonga kwa kamba aina ya manila.

Alikutwa amejinyonga juu ya mti uliopo kwenye pori la msitu unaomilikiwa na Kanisa Katoliki Abasia ya Peramiho karibu na maeneo ya Seminari Kuu ya Peramiho.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, aliiambia Nipashe jana kuwa tukio hilo lilitokea Mei 17 majira ya mchana.

Kamanda Maigwa alifafanua kuwa siku moja kabla ya tukio majira ya asubuhi, inadaiwa Sophia akiwa ameongozana na sista pamoja na wanafunzi wenzake wakielekea kanisani kusali, ghafla alimweleza sista kuwa kuna kitu amesahau bwenini, hivyo aliomba arudi kwenda kuchukua, lakini hakukurudi tena.

Kamanda Maigwa alisema baadaye walianza kumtafuta, lakini hakuweza kupatikana, na kwamba uongozi wa shule hiyo ulitoa taarifa polisi ya kupotelewa na mwanafunzi, huku jitihada za kumtafuta zikiendelea.

Hata hivyo, alisema juzi majira ya mchana, mwili wa Sophia ulikutwa ukiwa juu ya mti amejinyonga kwa kutumia kamba ya manila.

Alisema polisi walifanya uchunguzi wa awali na kubaini kuwa chanzo cha Sophia kujinyonga ni msongo wa mawazo, ambao ulimsababishia achukue maamuzi magumu baada ya ndugu zake kushindwa kumsaidia.

Aliongeza kuwa baadaye mwili wa marehemu ulikabidhiwa kwa ndugu, baada ya kufanyika kwa uchunguzi uliofanywa na polisi kwa kushirikiana na madaktari.

# Wadau wataja dawa kukabili soko la ajira

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wa maendeleo, wameshauri kuboreshwa kwa mtaala wa elimu ili usaidie kuinua zaidi ubora wa elimu nchini kwa kuendane na mabadiliko ya dunia ya sayansi na teknolojia yanayokua kwa kasi.

Mwakilishi kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Watoto (UNICEF), Dk. Daniel, Baheta, alisema kuendelea kutumia mtaala wa elimu usioendana na mabadiliko hayo ya sayansi na teknolojia kutachangia kutoa wanafunzi ambao hawataweza kushindana katika soko la ajira.

Alisema mabadiliko hayo ya kuweka mfumo mzuri wa elimu na maboresho yake yanatakiwa kuanzia katika elimu ya awali, msingi, sekondari hadi vyuo vikuu.

"Kwa sasa kuna ukuaji wa haraka wa sayansi na teknolojia na tunaona yameanza kutumika kwa kasi katika kila eneo, kwa hiyo si vibaya hata mitaala yetu katika sekta ya elimu ikaboreshwa kuendana na mabadiliko haya, bila kufanya hivyo naona tutakuwa bado tuko nyuma na hata wanafunzi watakaokuwa wanahitimu watashindwa kuuzika katika soko la ajira," alisema Dk. Baheta.

Dk. Baheta, pia alishauri kuendelea kuweka mazingira bora ya wanafunzi kujifunza kwa vitendo na kuelewa zaidi masomo yao.

Pia alisema katika kuwa na elimu bora kuna ulazima wa kuhakikisha suala la walimu wazuri na wenye weledi katika kazi ndio wanaoajiriwa.

Mdau mwingine wa Elimu, Edson Nyingi, alisema Tanzania imepiga hatua nzuri katika sekta hiyo japokuwa bado changamoto ndogo ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi ili kufikia malengo yanayokusudiwa.

Alisema ili kupiga hatua nzuri zaidi katika sekta hiyo ya elimu, serikali inatakiwa kufanya kazi kwa karibu zaidi na sekta binafsi kwa kuwekeza zaidi huko.

HABARI KITAIFA

# Vituo vya Covid viwanja vya ndege vyaongezwa

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imefanya maboresho katika upimaji wa COVID -19 kwenye viwanja vya ndege kwa kuongeza vituo kutoka viwili hadi 10.

Pia, imeboresha ulipaji kwa njia za kielektroniki ili kupunguza muda wa mlolongo wa upimaji.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Wizara hiyo, Prof. Abel Makubi, hatua hiyo imetokana na maoni ya abiria mbalimbali kuhusu uboreshaji wa ulipaji na upimaji wa COVID-19 Rapid Test katika viwanja vya ndege kwa wasafiri wanaoingia nchini.

Alisema hivi sasa mteja anatumia wastani wa dakika 15 kukamilisha mtiririko wa malipo na utoaji wa elimu kwa wasafiri juu ya kinga dhidi ya ugonjwa huo.

Prof. Makubi alisema kutokana na mwenendo wa ugonjwa huo duniani na uibukaji anuai mpya wa virusi hivyo katika baadhi ya nchi na kwa kuzingatia namna ambavyo ugonjwa huo unaambukiza wizara, ilielekeza wasafiri wote kutoka nje ya nchi wafanyiwe kipimo hicho pindi waingiapo nchini kupitia Mipakani, Viwanja vya Ndege vya Kimataifa na Bandari.

Akizungumzia kuhusu gharama za kipimo cha RT-PCR, kwa abiria wanaokuja Tanzania kutoka nje ya nchi, Katibu Mkuu huyo alisema abiria hao hutakiwa kupimwa na kulipia katika nchi yake anakotokea yaani kabla hajasafiri na hiyo ni mojawapo ya sharti la ndege anayopanda.



Wananchi wakiwa wamebeba mwili wa marehemu Denis Petro, baada ya kupewa amri na Jeshi la Polisi, ya kutoa katika ofisi ya Mtaa wa Nyambiti, Ilemela, mkoani Mwanza juzi. **PICHA: ROSE JACOB**

# Serikali yajivunia ongezeko la laini za simu na intaneti

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

LAINI za simu zinazotumika zimeongezeka kutoka 48,939,530 mwaka 2020 hadi kufikia laini 53,063,085 Aprili, 2021.

Aidha, watumiaji wa intaneti waliongezeka kutoka 26,832,089 mwaka 2020 hadi kufikia 29,071,817 Aprili, 2021 sawa na ongezeko la asilimia 8.3.

Akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi Waziri wa Mawasiliano na Tekonolojia ya Habari kwa mwaka 2020/21, Dk. Faustine Ndugulile, alisema watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa kwa njia ya mtandao wa simu wameongezeka 27,127,298 mwaka 2020 hadi kufikia 32,720,180 Aprili, 2021.

Alisema vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka 193 mwaka 2020 hadi 200 Aprili, 2021 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga vimeongezeka kutoka 43 mwaka 2020 na kufikia vituo 50 Aprili, 2021.

"Sekta ya Mawasiliano imekua kwa kasi ya asilimia 7.2 mwaka 2019, ikiwa ni ongezeko la upatikanaji na matumizi ya huduma za mawasiliano," alisema.

Waziri Ndugulile alisema laini za simu kwa njia ya kibiometria nchini hadi kufikia mwezi Aprili 2021, jumla ya laini 51,108,886; laini za simu ambazo zimesajiliwa kwa kitambulisho cha NIDA alisema kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 jumla ya laini za simu 8,436,805 zimesajiliwa ambapo ni ongezeko la asilimia 18.9 kutoka laini 44,626,280.

Kuhusu mkongo wa taifa wa mawasiliano umeendelea kutekelezwa ambapo jumla ya kilomita 409 zinaendele kujengwa katika mwaka wa fedha 2020/21.

Alisema Mkongo wa Taifa wenye urefu wa kilomita 105 kati ya Arusha na Namanga uliojengwa ardhini utahamishwa na kupitishwa kwenye nguzo za umeme wa Shirika la Umeme (TANESCO).

Dk. Ndugulile alisema ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano utahusisha pia ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za mawasiliano

katika eneo la Mtambaswala pamoja na vituo vitatu vya kuongeza nguvu ya Mkongo wa Taifa, na kwamba vituo viwili viko maeneo ya Kiyombo na Rungwa (Singida) na kituo kimoja eneo la Lupa Tingatinga (Mbeya).

# 'Tuma fedha namba hii' walivyowaliza wabunge

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

BAADHI ya wabunge jana walieleza bungeni jinsi walivyotapeliwa fedha kutokana na kupigiwa simu na watu wasiojulikana na wanaosema 'tuma kupitia namba hii'.

Akichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Tekonolojia ya Habari, jana, Mbunge wa Tabora Mjini (CCM), Emmanuel Mwakasaka, alisema kuna mtandao (aliutaja) wa simu akiona namba ya huduma kwa wateja hapokei kwa kuwa aliwahi kupokea na kutapeliwa zadi ya Sh. milioni 7.

"Serikali ifuatilie kwa kina licha ya kuwapo kwa usajili kwa alama za vidole, lakini bado kuna jumbe za tuma fedha kwenye namba hii," alisema. Alisema kama mtu amesajili laini yake na bado akaendelea kufanya utapeli bila kuchukuliwa hatua ni kuonyesha kuwa jambo hilo ni la kawaida kufanyika na wanaoumia ni wananchi.

Aidha, alisema mitandao ya simu inatumia simu za dharura kuweka matangazo kiasi cha mtu kushindwa kusaidiwa, huku akitolea mfano wa mtu anayepiga namba ya bure ya polisi kutoa taarifa ya kuvamiwa na majambazi anakutana na matangazo ambayo mteja hakuyataka.

Mbunge wa Msalala, Kassim Idd, alisema ni mwathirika wa wizi wa mtandao kupitia tuma kwenda namba hii.

"Tunaomba serikali ichukue hatua mimi ni mwathirika wa wizi mtandaoni, usalama wa fedha za wananchi ni mdogo na wengi wanapoteza fedha zao wakati serikali ipo," alisema.

Mbunge wa Jimbo la Makete, Festo Sanga, alieleza kupokea ujumbe kwenye simu yake ukimtaka kutuma fedha kupitia namna nyingine kwamba kuna mtu ana matatizo.

Aidha, wabunge wengi walitaka serikali kufuatilia wizi wa vifurushi ambao umekithiri kwenye mitandao mbalimbali.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya ***NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD, DOLPHIN GENERAL BUSINESS INTERPRISES C.LTD, CHAMPION AUCTION MART*** kwa niaba ya **Access Microfinance Bank Tanzania Limited** watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Magari na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne (14) tangu kutoka kwa gazeti hili, Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PAMBA | CHAMPION AUCTION MART | CHACHA/K,MARANYA | CHACHA/K, MARANYA | NYUMBA | KISHIRI MWANZA | 7/6/2021 |
| 2 | PAMBA | NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD | RWEGAYULA/E,ROSE | RWEGAYULA/E,ROSE | NYUMBA | NYASAKA MWANZA | 7/6/2021 |
| 3 | PAMBA | NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD | FOKOLO/R, MOHAMED | FOKOLO/R, MOHAMED | KIWANJA | MKOLANI MWANZA | 8/6/2021 |
| 4 | PAMBA | NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD | BUJIGWA/K, JASTINE | BUJIGWA/K, JASTINE | NYUMBA | MHONZE IGOMBE | 8/6/2021 |
| 5 | PAMBA | NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD | MAKONGOLO/J,ABEID | MAKONGOLO/J,ABEID | NYUMBA | NYASHO, B SIMIYU | 9/6/2021 |
| 6 | PAMBA | NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD | ALOYCE/S, DEUS | ALOYCE/S, DEUS | KIWANJA | MAINA MWANZA | 9/6/2021 |
| 7 | TABORA | CHAMPION AUCTION MART | MWINAMILA/S,PAUL | MWINAMILA/S,PAUL | FUSO TANDAM (FUSO LORI T187ARA | KAHAMA | 7/6/2021 |
| 8 | TABORA | DOLPHIN GENERAL BUSINESS ENTERPRISES COMPANY LTD | KAYANDA/RASHIDI,ALLY | KAYANDA/RASHIDI,ALLY | NYUMBA | USSOKE TABORA | 10/6/2021 |
| 9 | TABORA | DOLPHIN GENERAL BUSINESS ENTERPRISES COMPANY LTD | NASSORO/HARUNA, OMAYA | NASSORO/HARUNA, OMAYA | NYUMBA | CHESSA USSOKE TABORA | 10/6/2021 |
| 10 | TABORA | DOLPHIN GENERAL BUSINESS ENTERPRISES COMPANY LTD | KILASA/S, ALHAJI | KILASA/S,ALHAJI | NYUMBA | MARABI IPULI | 9/6/2021 |
| 11 | TABORA | DOLPHIN GENERAL BUSINESS ENTERPRISES COMPANY LTD | HUSSEN/J, AZZAMA | HUSSEN/J, AZZAMA | NYUMBA | MARABI IPULI | 9/6/2021 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa mara usomapo tangazo hili.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya fedha taslimu papo hapo na 75% baada ya siku 14 toka siku ya mnada kufanyika na ukishindwa kulipa malipo yaliyobaki mnada utarudiwa na fedha ulizo lipa hazitarudishwa.
3. Gharama za kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe, kumbuka vigezo na masharti kuzangatiwa

**MAWASILIANO**
**DOLPHIN GENERAL BUSINESS INTERPRISES C. LTD - 0754448694**
**NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD - 0754497396**
**CHAMPION AUCTION MART - 0716070188**
**WOTE MNAKARIBISHWA.**

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Udhibiti ujambazi upewe nguvu mpya

**USALAMA** na ulinzi wa mali za watu hauna mbadala. Yanapotokea matukio ya kutishia maisha na amani kila mmoja anapata hofu na kutaka kujua kinachoendelea ili kujihadhari.

Tukirejea hotuba ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoitoa kwa Jeshi la Polisi karibuni, anawaambia zipo habari za ujambazi kuanza kusikika na kuwauliza polisi kuwa kama hapo awali waliudhibiti ni nini kinachowakwamisha sasa?

Tunampongeza Rais kwa kuona hayo na pia tunawapongeza polisi na kamati za ulinzi na usalama kwa kazi kubwa inayofanyika ya kuhakikisha kuwa doria zinakuwapo wakati wote na uhalifu unadhibitiwa ama kukomeshwa.

Ingawa kazi inafanyika, ni ukweli kuwa maeneo kadhaa yanaeleza kuwapo kwa wizi, uporaji na hata matumizi ya silaha kwenye sehemu za burudani yakihusishwa na watu wanaodhaniwa kuwa ni majambazi.

Katika taarifa zinazozungumzwa mitaani, madereva wa bodaboda wanalalamikia kuporwa pikipiki. Wanasema wakati uporaji unafanyika kuna baadhi wamefunga kifaa cha kufuatilia mwenendo wa bodaboda au gari 'tracker' ambacho wanasema kinachomolewa na gari au boda kuibwa.

Maelezo yao yanasema kuwa pikipiki nyingi zimeibwa na hata magari na 'tracker' zimeng'ofolewa. Wizi unaofanyika na kuondoa vifaa hivyo unamaanisha kuwa waporaji wamejiandaa na kujipanga.

Wizi majumbani hasa kufuatilia runinga za 'flat screen' unatajwa, magari yaliyoegeshwa uwani kuchomolewa vifaa kama taa, usukani na vioo.

Watu wanaporwa njiani na vibaka, dawa za kulevya zinaanza kuingizwa ushahidi ukiwa jahazi lililokamatwa na shehena kubwa ya mihadarati.

Hata hivyo, wakuu wa polisi kwenye maeneo yenye ujambazi wako kimya. Taarifa hizo wananchi wanaona kuwa zinafichwa. Ukweli hausemwi pengine ni kulifanya jeshi lionekane kama linafanya kazi kwa ufanisi.

Pengine makamanda wanaogopa kuwa watakapotangaza masuala ya kuwapo uhalifu watatumbuliwa. Ukweli ni kwamba wanapotoa taarifa wananchi wanajipanga na kuanza kujilinda kupitia vikundi vya ulinzi shirikishi au sungusungu.

Polisi wafahamu kuwa wanapotoa taarifa za kuwapo uporaji wa pikipiki, bajaji na runinga nyumbani itawaamsha watu wakiwamo madereva kuwa makini zaidi na kuchukua tahadhari.


Taarifa pia zitaziweka familia zenye magari majumbani kuwa makini na hata ikibidi kuyawekea ulinzi na kubadilisha taratibu za kuyaegesha.

Tunaamini kuwa iwapo polisi watafunguka wananchi watakuwa tayari kuwapa taarifa za matukio ya uhalifu pengine hata kubainisha baadhi ya wana jamii ambao wanahusika au ni wahalifu.

Tunapowahamasisha polisi kuukabili uhalifu, tunapenda pia kuikumbusha serikali kwamba kazi hiyo ni ngumu. Wakati mwingine ni kifo kwa polisi wetu. Hivyo ni muhimu kuwapa motisha. Mshahara na posho zinazotosha kujikimu. Pengine ni wakati wa kutoa posho maalumu kwa vikosi vinavyohusika na kudhibiti ujambazi. Fedha hizo zipatikane kwa wakati na ziwe zinakidhi mahitaji isiwe ni posho ya Shilingi 20,000 ambayo katika hali ya kawaida haimfikishi polisi popote ukilinganisha na ugumu wa kazi anayofanya.

Aidha, pamoja na posho au malipo ya kazi hatarishi serikali iwapatie vifaa vya kisasa kuwakinga na wauaji. Vifaa hivyo vihusishe mavazi, magari, silaha na vyombo vya mawasiliano.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Itapendeza kama ushauri wa wataalamu afya utaafikiwa

Na Sabato Kasika

**BAADA** ya kamati ya kitaaluma iliyoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kutafiti kuhusu mwenendo wa ugonjwa wa Covid- 19, kuwasilisha ripoti kwake, kumekuwapo na mijadala mingi kwenye mitandao ya kijamii.

Katika mitandao hiyo wapo watu wanaopongeza mapendekezo ya kamati hiyo kwa serikali, yenye lengo kudhibiti ugonjwa huo nchini na wengine wakiyapinga hasa ya utoaji wa chanjo.

Baadhi ya mapendekezo hayo ni serikali kutumia vyombo vyake kuendelea na hatua kuelekea kuruhusu matumizi huru ya chanjo dhidi ya ugonjwa huo kwa kutumia chanjo zilizoorodheshwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Lengo la kufanya hivyo, ni kuwapa fursa ya kinga wananchi wake, kwa kuwa kupitia uchambuzi wa kamati, chanjo hizo zina ufanisi na usalama unaokubalika kisayansi.

Ingawa mapendekezo ya kamati hiyo ni mengi, hapo ndipo panaleta mjadala katika mitandao ya kijamii, baadhi ya watu wanapinga ushauri huo kwa madai kwamba chanjo hazifai.

Ni haki ya kikatiba kwa kila Mtanzania kutoa maoni yake, lakini kuna haja ya kutambua kuwa linapokuja suala la utafiti, maana yake ni kwamba huwa unapingwa na utafiti mwingine na wala siyo kupinga au kulalamika.

Inashangaza kuona wataalamu wamefanya utafiti kama walivyoelekezwa na Rais na kuja na mapendekezo au ushauri huo kwa serikali, halafu wanaibuka watu wengine kwenye mitandao ya kijamii wanaoanza kupinga.

Ni kweli kila mmoja ana haki ya kutoa maoni au kupinga jambo, kama analiona halijakaa sawa. Lakini, ieleweke inapokuja suala la utafiti, inapendeza iwapo utaheshimiwa na vyema mtu anayetaka kupinga, akatafiti kwanza na kuleta majibu yake.

Wataalamu hao walioteuliwa na Rais, wamefanya kazi kubwa na kuleta majibu ninayoamini yatasaidia kuwa salama na nimeushauri serikali kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha hatua zote za kinga katika ngazi zote.

Chini ya Prof. Said Aboud, kamati hiyo inaeleza kuwa hatua hiyo itasaidia kuepusha wimbi la tatu la ugonjwa, huku wakiwataka wataalamu wa afya kutimiza wajibu wao kitaalamu.

Hayo yanatakiwa kufanyika kwa kuzingatia weledi, miiko na maadili katika kuelimisha, kukinga na kutibu ugonjwa wa corona nchini.

Pia Tanzania ishiriki ipasavyo katika kuamua na itekeleze maazimio ya kikanda na kimataifa iliyoridhia katika jumuiya za Afrika Mashariki (EAC), Umoja wa Afrika (AU), SADC na WHO.

Serikali pia inashauriwa kuendelea kutoa fursa na kuwawezesha wanasayansi kufanya utafiti kwa kufuata miiko, maadili na taratibu zilizowekwa, ili kuimarisha kinga, tiba, uchunguzi wa maradhi ya Covid - 19 na athari zake katika jamii nchini.

Yapo mengi yaliyoshauri, ambayo kimsingi imekayakabidhi serikalini kwa lengo la kufanyia kazi ili kusaidia katika hatua zake za kudhibiti ugonjwa huo ili Watanzania waendelee kuwa salama.

Serikali inashauriwa kujengewa uwezo wa ndani wa utambuzi wa virusi anuai vinavyosababisha ugonjwa wa corona na magonjwa mengine ya kuambukiza na kutoa takwimu sahihi za ugonjwa huo kwa umma.


Lingine lililoshauriwa na kamati hiyo ni kwamba, kufanyike kwa umma na WHO ili wananchi wapate taarifa sahihi kutoka mamlaka za serikali na kuheshimu makubaliano na kanuni ambazo nchi iliridhia.

Hayo na mengine mengi yaliyoshauriwa na kamati hiyo, binafsi ninaona ni yana umuhimu mkubwa, hasa kwa kutambua kuwa waliofanya utafiti huo ni wataalamu wa afya na wanaheshimika kifani.

Ingekuwa vyema kama jamii itaendelea kujikita kwenye mijadala mingine ikiwamo ya kisiasa, kuliko kupinga utafiti wa kitaalamu wenye lengo la kuokoa maisha ya Watanzania, dhidi ya ugonjwa huo hatari.

Mtu asiyekuwa mtaalamu wa mambo ya sayansi kumpiga mwenye fani hiyo, ni sawa na kumwonea itakuwa vizuri iwapo taaluma za watu zitaheshimiwa kuliko kupinga tu bila ushahidi au utafiti.

HABARI KITAIFA




Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha (wa pili kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 56.07 kwa Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Nyamaganga Taraba, jana, kwa ajili ya malipo ya pili ya zao la pamba kwa wakulima wa Kishapu, waliouza zao hilo, kwa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), katika msimu uliopita. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Wanunuzi wa Pamba: Serikali imetushangaza

**Na Happy Severine,** BARIADI

WANUNUZI wa pamba wameshangazwa na maamuzi ya serikali katika msimu mpya wa ununuzi 2021/22 ya kuruhusu malipo ya wakulima kulipwa fedha taslimu badala ya kulipiwa benki.

Wamesema kuwa maagizo ya serikali kabla ya msimu kuzinduliwa yaliyotolewa na mawaziri kwa nyakati tofauti yalikuwa malipo ya wakulima katika msimu huu yafanyike kwa njia ya benki au mitandao ya simu. Akizungumza na waandishi wa habari jana Katibu wa Chama cha Wanunuzi wa zao hilo nchini (TCA), Boaz Ogolla, alisema wameshangazwa na maamuzi hayo, ambayo yanaendelea kuweka mazingira magumu ya pesa na wakulima.

Ogolla alisema walikuwa wamejipanga kulipa wakulima kwa njia za benki au mitandao ya simu na malipo yangefanyika kwa haraka, lakini mwongozo wa serikali ambao uliletwa uliruhusu malipo ya mkono kufanyika. "Mwongozo ambao ulikuja umesema malipo yanaweza kufanyika kwa njia ya pesa taslimu, benki au simu, wakulima na Amcos wao ndiyo waamue walipwe kwa njia gani, baada ya kuanza kununua wakulima wote wanataka kulipwa kwa mkono," alisema Ogolla.

Alisema baada ya mwongozo wa serikali kutolewa, Amcos nyingi zimeegemea upande wa pesa taslimu, na hakuna amcos ambayo imeomba malipo ya wakulima wake yapitie benki au kwa kutumia mitandao ya simu.

Ogolla alieleza kuwa pesa kulipwa kwa njia ya taslimu, itasababisha matatizo ambayo yalikuwapo huko nyuma yaweze kujirudia ikiwemo wizi wa pesa za wakulima ikiwa ni pamoja na upotevu wa pesa za wanunuzi.

liongeza kuwa Amcos nyingi hazina uwezo wa kutunza pesa nyingi, hivyo kusababisha usalama mdogo wa pesa zao kama wanunuzi lakini pia pesa za wakulima ikiwa Amcos itaachiwa pesa nyingi na zikapotea.

" Serikali iliagiza benki kuwafungulia wakulima akaunti na benki nyingi zilifanya hivyo, kwa uamuzi huu hizo akaunti hazitafanya kazi tena hiyo ni hasara kwa benki, lakini usalama wa pesa zetu hautakuwepo," alisema Ogolla.

# TTCL yaelemewa kwa madeni, wabunge wataka yalipwe haraka

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

KAMATI na wabunge wameitaka serikali kulipa madeni na kuongeza mtaji kwa Shirika la Simu Tanzania (TTCL), ambao limeelemewa kiasi cha kudumaa na kushindwa kushindana na kampuni binafsi.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Anne Malecela, alisema hadi Januari, 2021 Sh. bilioni 20.1 ikiwa ni madeni ya zamani ambayo yanatokana na kutumia huduma mbalimbali za serikali na taasisi zake.

Alisema ni muhimu sana serikali iweke mkazo kwa vyombo vyake vyote kulipa madeni yanayodaiwa na TTCL ambayo hadi Machi, 2021 yameripotiwa kufika Sh. bilioni 14.8.

Alisema kutokuwapo kwa fungu la fedha za uendeshaji na usimamizi wa Mkongo wa Taifa kumsababisha TTCL kutumia fedha zake za mapato ya ndani kwa ajili ya Mkongo pasipo kurejeshewa.

Alisema hadi Desemba 2020, TTCL inaidai wizara jumla ya Dola za Kimarekani 68,309,414.30, na kuitaka serikali kuangalia suala hilo kwa jicho la pekee.

"Serikali iangalie namna itakavyoweza kusaidia TTCL kwenye Sheria za Manunuzi ili ziweze kubadilika ili TTCL iweze kwenda kasi na kushindana na kampuni nyingine za mawasiliano," alisema Malecela.

Aidha, alisema kwa mwaka 2020/21 TTCL lilikadiria kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 199.2 kutokana na huduma za simu, data na kupangisha maeneo kwa ajili ya vyombo vya mawasiliano.

Alisema sababu za TTCL kutokufikia malengo ya makusanyo ni kukosa fedha kwa ajili ya uwekezaji kutoka kwenye vyanzo vyake. Aidha, alisema pamoja na changamoto hizo katika mwaka wa fedha 2021/2022, TTCL inakadiria kukusanya Sh. bilioni 232.4, na kwamba ni ongezeko la asilimia 17 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo mwaka 2020/2021.

Alibainisha changamoto nyingine ni mtaji mdogo kwa ajili ya uwekezaji na kushindwa kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia yanayokwenda sambamba na kasi ya uwekezaji.

Nyingine ni sheria ya manunuzi kwa mashirika ya umma ambayo inaleta urasimu unaokinzana na ushindani wa kibiashara.

Mbunge wa Ilala, Jerry Silaa, alisema kama serikali inataka kufanya biashara ifanye na kama hawezi iiachie sekta binafsi, huku akitolea mfano wa makadirio ya wateja milioni moja kwa TTCL wakati kampuni binafsi zina wateja milioni 15.

Mbunge wa Viti Maalum, Hawa Mchafu, alisema serikali inaikamua TTCL bila kuilisha, na kwamba kama wanataka shirika hilo kujiendesha kwa ushindani ni lazima wawekeze mtaji wa kutosha.

Mbunge wa Nanyamba, Abdallah Chikota, alisema: "Inashangaza kuona serikali inadaiwa na TTCL wakati bajeti zao zinakuja bungeni tunapitisha, wawakatie huduma kama binafsi wanavyofanya kama hawalipii huduma wanazotumia hakuna namna ni kukata tu, vinginevyo litakufa."

# EU yapiga jeki mabadiliko tabianchi

**Na Romana Mallya**

UMOJA wa Ulaya (EU) umesema kwa kiasi kikubwa uchumi wa Tanzania unategemea shughuli za kilimo zinazotegemea mvua ambazo mabadiliko ya tabia nchi imeziathiri hivyo kwa kushirikiana na serikali wapendekeza miradi itakayosaidia wananchi.

Balozi wa EU nchini, Manfredo Fanti, aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa maonyesho na kampeni ya miezi sita wali yoandaa ili kuhamasisha kupambana na mabadiliko ya tabia nchi Tanzania.

Alisema matukio ya hali ya hewa yanatarajiwa kuongezeka na kuathiri uzalishaji wa kilimo, mifumo ya ikolojia, bioanuai na miundombinu.

Balozi Fanti alisema kampeni hiyo ambayo imebebwa na jina la Resilience to Climate Change (kustahimili mabadiliko ya tabia nchi), wamedhamiria kuisaidia Tanzania njia za uhamasishaji wa kitaifa wa kupambana na tatizo hilo unaosababisha uharibifu wa mazingira na kupotea kwa bioanuwai.

"Mabadiliko ya tabia nchi hayapo Tanzania peke yake hili ni tatizo kubwa linaloikabili dunia kwa sasa. Mpango wa kijani wa EU umeainisha hatua za kuchukuliwa ili kukuza matumizi bora ya rasilimali kwa kuhamia kwenye uchumi safi wa mzunguko ambao unarejesha bioanuai na kupunguza uchafuzi wa mazingira," alisema.

Alisema EU inashirikiana na nchi 11 wanachama na asasi za kiraia katika kuhamia kwenye kilimo kinachozingatia tabia nchi, nishati mbadala, ukuaji mdogo wa kaboni kulingana na malengo endelevu, matumizi bora ya nishati na usimamizi endelevu wa rasilimali. Meneja wa Mradi kutoka Umoja wa Ulaya Tanzania anayeshughulikia masuala ya mabadiliko ya tabianchi, Mathew Mpanda, alisema EU imekuwa mshirika mkubwa wa Tanzania wa kupambana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kushirikiana na wizara mbalimbali ipo miradi inayotekelezwa. Mpanda alisema kwa kipindi cha miaka 10, Umoja wa Ulaya umewekeza Euro milioni 10 (zaidi ya Sh. bilioni 25) kwenye masuala ya tabia nchi.

# Mapitio sera ya sayansi mbioni

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema iko katika hatua ya mwisho ya kufanya mapitio ya sera ya sayansi na teknolojia ili iendane na hali ya ubunifu wa kidigitali na kuzifanya ziuzike.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga wakati akifungua wiki ya ubunifu jijini Dar es Salaam.

Alisema mapitio ya sera hiyo itasaidia kuwatambua wabunifu na kuwaendeleza ili kuleta mabadiliko ya kidigitali.

Aliiagiza Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH ), kuweka kituo kitakachowakutanisha wabunifu na bunifu mbalimbali ili watu wakitumie kujifunza.

Kipanga alisema kuwa serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara katika kuchangia ukuaji wa uchumi kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa katika teknolojia.

Alisema serikali itaendelea kuratibu, kusimamia na kuzifanya bunifu zote kuwa bidhaa na kwamba ni wakati wa wabunifu hao kubuni vitu vyenye tija ili kutatua changamoto kwenye jamii.

"Tutaendelea kuimarisha miundombinu yote ya mawasiliano kwani ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi. Lakini serikali pekee haitaweza kuleta mabadiliko endapo hatutashirikisha wadau, wabunifu na wafadhili," alisema Kipanga.

Pia alisema ubunifu umechangia katika kuongeza ajira kwani huduma nyingi zinatolewa kwa njia ya mtandao ikiwamo ulipaji wa bili mbalimbali maji, umeme na leseni za biashara.

Mkurugenzi Mkazi wa HDIF, Joseph Manirakiza, alisema mfuko huo umechangia ukuaji wa masuala ya ubunifu nchini kwani ilifadhili miradi 48 kutoka kwa wabunifu wadogo 55 na matumizi kupitia mashindano kwa kushirikiana na COSTECH.

Manirakiza alisema katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano umeelezea umuhimu wa kukuza ubunifu na teknolojia katika kuongeza uzalishaji na kutoa nafasi katika kuchangia ukuaji wa uchumi kidigitali.

# Kilosa waamriwa kuhama mabondeni

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI wilayani Kilosa mkoani Morogoro, imewataka wananchi wanaoishi mabondeni kuondoka mara moja na kuhamia katika maeneo maalumu yaliyotengwa na halmashauri hiyo, kuepukana na athari za maafa ya mafuriko. Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa wilaya hiyo, Adam Mgoyi, wakati wa ufunguzi wa semina ya siku tatu ya kuongeza uelewa wa jamii kuhusu maafa yatokanayo na mafuriko.

"Nawataka wananchi wote waliojenga katika mapito ya maji, wanazuia maji kufuata mkondo wake na kusababisha maafa ya mafuriko na wale wa mabondeni wahamie maeneo ya miinuko," alisema.

Alisema hata wale waliojenga kwenye maeneo ya kilimo na waliogeuza maeneo ya kilimo kuwa makazi badala ya kujenga makambi ya muda kwa ajili ya kusimamia mashamba yao warudi katika maeneo waliopatiwa.

Mgoyi alisema kumekuwapo na utamaduni wa wananchi kutaka fidia maafa yanapotokea bila kutambua wao ni sehemu ya visababishi vya maafa hayo huku akiwasisitiza kutokuwapo fidia kwa mwananchi ambaye atakaidi maagizo ya serikali.

Alifafanua kuwa serikali humo imeanza mpango mkakati wa kuhuisha miundombinu ya maji ili kusaidia kukabiliana na kasi ya maji ambayo inaleta athari kwa wananchi wilayani humo.

Mkurugenzi Msaidizi Ofisi ya Waziri Mkuu Kituo cha Operesheni Mawasiliano ya Dharura, Selestine Masalamado, aliwataka wananchi wilayani humo kuchukua hatua za kupunguza athari za maafa zikiwamo kutochimba madini kando ya mito, kutofanya shughuli za kilimo na ufugaji kando ya mito hiyo.

Naye Katibu Tawala Msaidizi (Mipango na Uratibu) ambaye ni Mratibu wa Usimamizi wa Maafa Mkoa wa Morogoro, Hanza Ndossa, alisema elimu hiyo ni muhimu kwa wananchi hao kwa kuwa Wilaya ya Kilosa ina kata 40, huku 11 kati ya hizo zinaathirika na mafuriko ambapo kijiji cha Kitete huathiriwa na maafa na kwamba Machi 2020 kaya takribani kaya 791 ziliathirika kwa maafa ya mafuriko.

Akizungumza kwa niaba ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wahamaji (IOM), Reuben Mbugi amehakikishia Serikali ya Tanzania kuwa wataendelea kushirikiana nao katika kuijengea jamii uwezo wa kukabiliana na maafa yatokanayo na mafuriko.



Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya Tanzania Breweries Ltd (TBL), Philip Redman, akizungumza na wageni waalikwa jijini Dar es Salaam jana, wakati wa hafla ya uzinduzi wa ripoti ya EY kuhusu mchango wa kampuni hiyo katika kukuza uchumi nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TASAC yaanika sababu ajali za majini

**Na Christina Mwakangale**

ASILIMIA 85 ya ajali zinazotokea majini, ikiwamo baharini na ziwani, hutokana na sababu za kibinadamu ikiwamo uzembe na vikwazo vya lugha ya mawasiliano.

Meneja wa Huduma za Mabaharia na Mafunzo kutoka Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Iroga Nashon, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, kwenye semina ya wanahabari kukuza uelewa wa shughuli za majini.

Alisema kutokana na mabaharia wanaoongoza meli kutoka nchi tofauti kwa ajili ya kusafirisha mizigo, kutoelewa lugha ya mahali husika, huwa sababu ya ajali hizo.

"Uzembe wa mabaharia kutoelewana lugha za mawasiliano, utakuta hamwelewani, huyu anasema nipishe upande huu kumbe hamjaelewana, ajali inatokea.

"Mara nyingi huwa tunauliza bahari ni pana kuliko barabara, iweje ajali itokee? Jibu ni kwamba kunatokea kutoelewana kati yao," alisema Nashon.

Kadhalika, Nashon alifafanua kwamba ajali nyingine hutokana na uundwaji duni wa meli pamoja na kupakiwa mzigo kupindukia bila kufuata vipimo vilivyowekwa kisheria.

"Kwa kiwango kikubwa meli imeundwa ili ielee kwa muda wote baharini, hata inapotokea dharura itaelea tu, vilevile ikizima inaelea. Kinachosababisha meli ya abiria kuzama haraka ni taharuki miongoni mwa abiria, wakidhani hatari inapotokea wanazama papo hapo," alisema.

Pia alisema vikwazo vilivyopo majini ni uchafuzi wa mazingira, ikiwamo taka na mafuta kuvuja kutoka kwenye meli na kuathiri viumbe hai.

Ofisa Uhusiano wa Jamii TASAC, Nicholaus Kinyariri, alisema tangu mwaka 2018 hadi 2020, shirika hilo limefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali, ikiwamo kutoa gawio kwa serikali ambalo ni takribani Sh. bilioni 40 hadi sasa.

Alisema pia shirika hilo, limefuta tozo saba ambazo kati yake zilikuwa kikwazo kwa wateja pamoja na kusimamia ipasavyo shughuli za utendaji na utekelezaji majukumu ya shirika hilo.

HABARI KITAIFA

## Wanaovujisha siri za serikali kukiona

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema kumekuwa na ongezeko la uvujaji wa taarifa zake za siri na kuiagiza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kushirikiana na Mfumo wa Kukusanya Mapato Serikalini (GePG) kuwafuatilia wale wote wanaohusika na wachukuliwe hatua.

Pia, imesema zipo taasisi zikishirikiana na baadhi ya wadau au wafadhili wao zimekuwa zikijaribu kuchezea mifumo ya serikali ya kimtandao ili ionekane dhaifu, itumike yao waliyoianzisha na kuonya kuwa kufanya hivyo ni kosa la uhujumu uchumi na watachukuliwa hatua.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzingatiaji wa sheria ya serikali mtandao namba 10 ya mwaka 2019 na kanuni zake za mwaka 2020.

Alisema sheria hizo zinaainisha utaratibu maalum wa kisheria na usimamizi wa utaratibu na uendeshaji wa jitihada za serikali mtandao katika taasisi za umma na kutatua matatizo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na uendeshaji wake.

Alisema licha ya kuwapo kwa sheria hizo lakini hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la uvujaji siri za serikali na kuagiza kufanyike ufuatiliaji wa usalama wa mifumo iliyopo.

"Tumeshaagiza watu wa mfumo wa GePG washirikane na TCRA kuhakikisha wanadhibiti uvujaji wa siri na utolewaji wa taarifa ambazo hazistahili kwenda moja kwa moja. Kwa kutumia mifumo tuliyonayo tutawabaini wote wanaohusika kutoka taarifa zikiwamo za uchochezi za kupotosha au kuleta taharuki kwa jamii," alisema.

Alisema wanafahamu kuna taasisi za serikali kwa kushirikiana na wadau wao wanataka kujitoa katika matumizi ya mifumo ya mamlaka ya serikali ya mtandao GePG na kuwakumbusha kuwa kufanya hivyo ni kosa.

"Ninatoa rai na onyo wakuu wote wa taasisi za serikali hakuna taasisi yoyote wala ofisi yoyote ya serikali ambayo inaruhusiwa kujitoa kwenye mifumo inayosimamiwa na mamlaka ya serikali, ni kinyume cha Sheria namna 10 ya mwaka 2019 na kanuni zake za mwaka 2020.

"Ninawaonya wakuu wote wa taasisi ambao wanaanzisha mifumo yao ya kimtandao bila kuzingatia kanuni, sheria na taratibu, GEPG ifuatilie taasisi zilizoanzisha mifumo yake na hawakupata kibali au kuzingatia matakwa ya sheria," alisema.

# Waziri aunda Kamati ya Elimu Muungano

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, ameteua wajumbe saba wa kamati itakayofanya kazi ya kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uboreshaji wa elimu katika Muungano.

Akizungumza na waandishi wa habari visiwani Zanzibar, Jafo alisema juzi kuwa uteuzi huo umefanyika ikiwa ni hatua ya kushughulikia maoni yaliyotolewa na wadau mbalimbali kuhusu tofauti ya ufaulu wa wanafunzi wa Shule za Sekondari za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa matokeo ya kidato cha nne na sita.

Pamoja na maoni hayo alisema wabunge mbalimbali wamekuwa wakiwasilisha hoja hiyo wakati wa mjadala wa bajeti ya mwaka 2021/22 wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

Jafo aliipa kamati hiyo siku 35 kukamilisha kazi ya kushughulikia maoni hayo na kuwasilisha taarifa kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ili kwa kushirikiana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi wakae na mawaziri wanaohusika na masuala ya elimu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuwashauri namna bora ya kuboresha elimu pande zote mbili za Muungano.

Waziri Jafo aliwataja wajumbe walioteuliwa kuwa ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Taaluma, Utafiti na Huduma kwa Umma), Prof. Alexander Makulilo ambaye atakuwa Mwenyekiti na Makamu wake ni Mbunge wa Viti Maalum kutoka Zanzibar, Najma Murtaza Giga ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

Wajumbe watakaounda kamati ni mdau wa elimu sekta binafsi Abdulmarik Mollel, Mkurugenzi wa Uratibu wa Shughuli za Serikali, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Khalid Bakari Hamrani, Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA), Dk. Charles Msonde,

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Gerald Mweli na Mkufunzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma Zanzibar (IPA), Said Hamad Shehe.



Mkurugenzi na Mhandisi wa Tanzania Building Works, Mohamed Noray, akipata maelezo kutoka kwa Msimamizi wa ufumaji katika kiwanda cha ushonaji nguo cha Jeshi la Polisi Kurasini, Musa Chitande (kulia), wakati wa uzinduzi wa kiwanda hicho, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki yatoa bil. 5/- kukopesha bodaboda

**Na Richard Makore,** MWANZA

BENKI ya NMB imetenga Sh. bilioni 5 kwa ajili ya kutoa mikopo ya bodaboda na bajaji kwa waendeshaji wa vyombo hivyo kupitia umoja wao hapa nchini.

Akizungumza katika uzinduzi wa mikopo hiyo kwa vijana waendesha bodaboda na bajaji jijini Mwanza, Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki ya NMB, Ruth Zaipuna, aliwataka wanufaika kujitokeza na kuchangamkia fursa hiyo.

Alisema ikiwa vijana na watu wengine waliojiunga katika umoja wa waendesha bodaboda na bajaji watajitokeza na kuchangamkia fursa hiyo, NMB inaweza kuongeza kiwango cha utoaji mikopo.

Zaipuna alisema kwa mara ya kwanza walizindua huduma hiyo jijini Dar es Salaam na kwamba jana waliingia jijini Mwanza ili kuhakikisha vijana wanatumia fursa hiyo kupata mikopo na hivyo kujiajiri wenyewe.

"Hatutaki mikopo hii iwe mizigo kwenu bali baraka kwenu na NMB imedhamiria kufika katika mikoa mingine hapa nchini kwa ajili ya utoaji wa mikopo hii,'" alisema. Alisema, hatua ya utoaji wa mikopo hiyo ni ombi la serikali la kuomba wasaidie vijana kupata mikopo ya bodaboda na bajaji na kwamba wameamua kulitekeleza kwa vitendo.

Mkuu wa kitengo cha wafanyabiashra wadogo wa NMB, Filbert Mponzi," alisema benki hiyo imeandaa mfumo wa malipo ya Master Boda QR utakaomuwezesha mteja kumlipa bodaboda nauli.

Alisema ili kupata mkopo wa bodaboda, lazima kila mwanachama wa umoja wa waendesha bodaboda afungue akaunti ya NMB na kuanza kuingiza fedha anayolipwa na wateja kama nauli walau kuanzia miezi mitatu.

Aidha, alisema kila mwezi wanatoa mikopo ya wajasiliamali hapa nchiniinayofikia Sh. bilioni 40.

Aliwaomba Watanzania kujiunga katika vikundi na kufungua bima ambayo itawasaidia wanapopata misiba ya ndugu wa karibu.

Alisema kiwango cha kila mwanachama katika kikundi ni Sh. 2,000 kwa mwezi na kwamba ikiwa atafariki NMB itatoa Sh. milioni 5.

Aidha, alisema bima hiyo pia itahusisha mwanachama kufiwa na mke na watoto ambapo pia NMB itatoa rambirambi.

Katibu wa waendesha bodaboda mkoani Mwanza, Samue Anthony, alisema wameweza kuunganisha vijana 100 waliokuwa wakitumia madawa ya kulevya na sasa wamekuwa watu wema ambao wanashirikiana nao.

Aliomba NMB kuendelea kuwapa elimu kuhusu namna bora ya matumizi bora ya fedha watakazopata kupitia vyombo hivyo ili wanifaike.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Salum Kali, aliwahakikishia usalama waendesha bodaboda na bajaji muda wote watapokuwa kazini.

HABARI BUNGENI

# Serikali yatoa mabilioni kumaliza uhaba wa dawa

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imepatiwa mwezi huu Sh. bilioni 80 na serikali kwa ajili kununua dawa ili kupunguza uhaba uliopo kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, aliyasema hayo jana bungeni, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Grace Tendega.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema kumekuwa na kero ya huduma za afya katika zahanati hasa ukosefu wa dawa pamoja na ukosefu wa huduma bure kwa wazee, watoto na wajawazito.

"Je, ni lini serikali itahakikisha Sera ya Afya inatekelezwa bila tatizo lolote?" Mbunge huyo alihoji.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema ili kukabiliana na tatizo hilo, mwezi huu serikali imeipatia wizara hiyo fedha hizo kwa ajili ya kununua dawa kwenye vituo hivyo.

"Dawa zitakazonunuliwa zitapunguza tatizo la dawa kwa kiasi kikubwa na serikali inaendelea kudhibiti mianya ya upotevu wa dawa ili kuhakikisha kuwa dawa zinazonunuliwa zinawanufaisha walengwa," alisema.

Vilevile, alisema katika kuhakikisha inaboresha upatikanaji wa dawa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini, serikali imeongeza bajeti ya bidhaa za afya kutoka Sh. bilioni 31 katika mwaka wa fedha 2015/16 hadi Sh. bilioni 270 katika mwaka wa fedha 2020/21.

"Ongezeko hilo la bajeti na fedha inayotolewa limesababisha hali ya upatikanaji wa dawa za msingi kuongezeka kutoka wastani wa asilimia 35 hadi asilimia 90," alisema.

Hata hivyo, alisema kuna kero ya upatikanaji wa dawa za makundi maalum nje ya dawa za msingi hasa katika ngazi ya zahanati ambapo dawa nyingi zinazohusu magonjwa ya uzeeni zinaangukia kwenye kundi hilo.



Baadhi ya wabunge wakiwapongeza Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Leonard Chamuriho na Manaibu wake, Mwita Waitara na Mhandisi Gofrey Msongwe, baada ya bajeti ya Wizara hiyo ya mwaka 2021/2022 kupitishwa, bungeni jijini Dodoma juzi usiku. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## 'Serikali haijazuia uvuvi wa kamba koche'

SERIKALI imeliarifu Bunge kuwa haijawahi kuzuia uvuvi wa kamba koche.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kibiti (CCM), Twaha Mpembenwe.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji ni lini serikali itatoa uamuzi wa kuwaruhusu wavuvi wa kamba koche kuvua kuanzia mwezi Desemba hadi Julai kila mwaka.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ulega alisema kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya Mwaka 2003 pamoja na kanuni zake za nwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2020, serikali haijawahi kuzuia uvuvi wa kamba koche.

Hata hivyo, alisema serikali imeweka utaratibu kwa ajili ya uvuvi wa kambamiti kwa wavuvi wadogo na wakubwa.

"Uvuvi wa kambamiti kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo unaruhusiwa kufanyika kuanzia mwezi Machi hadi Septemba kila mwaka kwa ukanda wa kaskazini unaohusisha Wilaya za Bagamoyo, Pangani na Chalinze na kuanzia mwezi Aprili hadi Agosti kila mwaka kwa ukanda wa kusini unaohusisha Wilaya za Mkuranga, Kibiti na Kilwa," alisema.

Ulega alisema kipindi kilichobaki kimeachwa ili Kambamiti wazaliane na kukua.

"Uamuzi huu umefanyika baada ya taarifa za utafiti wa kisayansi na kuzingatia uendelevu wa rasilimali hii," alisema.

Ulega alisema serikali imekuwa ikisisitiza kwa wadau wote wa uvuvi hususani uvuvi wa kambamiti kufanya shughuli zao kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo kwa lengo la kuwa na uvuvi endelevu kwa maslahi mapana ya vizazi vilivyopo na vijavyo.

# Mbunge apata mwarobaini ujenzi viwanda vya korosho

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, ameitaka serikali kuweka vivutio maalum ili kuvutia wawekezaji kwenye viwanda vya kubangua korosho.

Akiuliza maswali bungeni jana, Chikota alisema utaratibu wa mfumo wa soko la awali hukutanisha wenye viwanda na wakulima lakini hauna ushindani kwa sababu bei ni ndogo na wakulima hawavutiwi kupeleka bidhaa zao wanaona kama kangomba.

Alihoji serikali ina mpango gani wa kujazia upungufu kwenye bei halisi, kwa bei ile inayotolewa na wawekezaji ili kuhakikisha wawekezaji wanapata korosho katika soko.

"Viwanda hivi vimeajiri vijana na kinamama wengi na vinafanya kazi chini ya uwezo wake kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo ya ukosekanaji wa malighafi sababu hawapati korosho mnadani," alisema.

Alihoji serikali inatoa kauli gani kwa wawekezaji waliofungua viwanda nchini na wanaotarajia kuja kuwekeza.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji, William Ole Nasha, aliahidi serikali itaboresha mfumo wa soko la awali kwa wabanguaji wa ndani wa zao hilo ili uvutie na wakulima wasione kama wanatumia mfumo wa kangomba.

Ole Nasha alimhakikishia mbunge huyo kuwa kwa sababu ndio mfumo huo umeanza utaboreshwa ili kuvutia wakulima.

Aidha, alisema serikali inafikiria namna bora ya kuhakikisha korosho inapatikana ili ajira zitolewe kwa vijana.

Awali, Naibu Waziri huyo alisema serikali inatekeleza mpango wa uhamasishaji wa kilimo cha korosho katika mikoa yote inayostawisha.

Alisema lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora, huduma za ugani na pembejeo ili kuimarisha upatikanaji wa malighafi kwa viwanda nchini.

"Hadi sasa takribani mikoa 20 inazalisha zao hilo kwa viwango tofauti na msimu wa mwaka 2020/21 uzalishaji ulikuwa tani 200,010 na kuipatia nchi kiasi cha Sh. bilioni 477," alisema.

Alifafanua kuwa ili kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya kubangua korosho, serikali imeweka vivutio mbalimbali ikiwamo vivutio visivyo vya kikodi kama vile kuweka mfumo wa soko la awali kwa wabanguaji wa ndani kuanzia mwaka 2020.

"Lengo ni kuwawezesha kununua korosho bila kushindana na wanunuzi wanaosafirisha korosho ghafi kwenda masoko ya nje ya nchi na kuwahakikishia malighafi kwa bei nafuu," alisema.

Kadhalika, alisema katika mnada huo jumla ya tani 2,021.7 zimenunuliwa na viwanda tisa vilivyoshiriki soko hilo la awali.

Alibainisha serikali imeweka pia vivutio vya kikodi kwa viwanda vya kubangua korosho kupitia Sheria ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje Sura 373 ikiwamo msamaha wa Kodi ya Kampuni (Corporate Tax) kwa miaka 10.

"Msamaha wa asilimia 100 wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa bidhaa za mtaji, msamaha wa asilimia 100 wa Kodi ya Zuio kwa riba ya mikopo kutoka nje, pango na gawio na msamaha wa asilimia 100 wa Kodi ya Ushuru wa Forodha kwa mitambo na vifaa," alisema.

Alisema kupitia utaratibu huo, jumla ya viwanda vitano vimesajiliwa na Mamlaka ya Uwekezaji kwa Mauzo Nje (EPZ).

Alisisitiza serikali itaendelea kubuni na kuweka vivutio mbalimbali vya kikodi na visivyo vya kikodi ili kuvutia zaidi uwekezaji ikiwamo kutenga maeneo maalum kwa ajili ya ujenzi wa viwanda kwenye halmashauri zinazolima korosho nchini.




**Habari zote na Augusta Njoji**

ama
ALHAMISI MEI 20, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**MAGEUZI YA DEMOGRAFIA**
**Kudhibiti uzazi China kunavyomaliza idadi vijana, watoto, nguvukazi taifa**


Ukurasa 12

**MAMBO YA JKCI...**
**Prof. Janabi: Haya ndio mapinduzi namna tunavyotibu umeme moyo**

# Wanaharakati walivyoamka na yao kujadili bajeti ya Waziri Gwajima

**Na Yasmine Protace**

AFYA ni nini? Jibu la jumla linaangukia katika tafsiri ya jumla kwamba, ni maisha ya kila siku yanayohusisha mwili wa mtu, ikianza na nyenzo kama moyo, ubongo, viungo vingine na mazingira yanayomzunguka.

Hapo mtu kila akifanyacho, inabeba tafsiri katika maisha yake. Ni namna gani anahusika au kutohusika nayo, inakuja na tafsiri ya ama kumjenga au kumbomoa kimaisha kwa kuangukia tafsiri ya afya.

Namna afya hiyo na vigezo vyake vinahudumiwa hata kuleta sura ya matokeo, iwe chanya au hasi, hutegemea tofauti kati ya mtu mmoja na mwingine, katika uelewa wake, anavyochukulia uzito na tafsiri kulingana na tofauti kati yao.

Hivyo, jamii inatakiwa kuzingatia masuala ya afya kuepukana na kupata magonjwa ya aina yoyote, jambo ambalo nchini serikali kupitia Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, ina hatua inazochukua kufanikisha mtazamo huo.

Mojawapo inayojulikana ni haja ya kuwapo bima ya afya inayomfikia kila mtu nchini, ambayo waziri mwenye dhamana, Dk. Dorothy Gwajima, katika mapendekezo ya mapato na matumizi ya mwaka ujao wa fedha, ana orodha ya namna yaliyoandaliwa kuboreshwa kwa ajili ya kuingizwa katika upatikanaji bima.



Ofisa Programu kutoka TGNP Mtandao, Anna Sangai. **PICHA: MTANDAO**

**MAONI YA WADAU**

Baada ya kuwasilishwa makadirio hayo ya mapato na matumizi hivi karibuni, wadau wa Semina za Jinsia na Maendeleo GDSS zinazofanyika jijini Dar es Salaam, nao waliwasilisha mapendekezo, wakiwa na mitazamo kadhaa.

Janeth John, mshiriki wa GDSS anakiri kusikia maelezo ya makadirio ya mapato na matumizi, akiwa na ufafanuzi: "Inatakiwa elimu ya ukatili ianze kutolewa shule ya msingi na kuendelea ili watoto wanapofanyiwa ukatili waweze kutoa taarifa."

Janeth anasisistiza umuhimu wa nyumba za ibada na mikusanyiko ya watu kama makundi ya vikoba kutolewe elimu stahiki, kuoanisha mahitaji ya kiusalama kwa umma.

Mshiriki huyo anasema, uboreshaji wa miundombinu katika hospitali na vituo vya afya unapaswa kuangalia namna baadhi ya maeneo na hasa vijijini, ambako miundombinu yake haikidhi mahitaji ya umma na kusababisha malalamiko mengi ya jamii.

Ofisa Programu kutoka TGNP Mtandao, Anna Sangai, anasema asasi yake inayotumia utetezi wa haki za kijinsia na watoto, anaeleza wanavyovutiwa na maboresho makubwa ambayo wizara yenye dhamana na afya, imeshajipanga kuyafanya.

Anasema katika miundombinu, suala la kufunguliwa vituo vya afya pasipo kukamilika kwa miundombinu na mahitaji muhimu katika uendeshaji wake, ni jambo linalochangia malalamiko kutoka kwa umma wa walengwa.

"Tusikimbilie kufungua vituo vya afya, kama vinakuwa bado inabidi kusubiri vikamilike, ili viweze kutoa huduma zilizo sahihi," anafafanua, Anna, msomi mwandamzi katika stadi za ualimu na taaluma ya maendeleo.

Mdau mwingine, Nyajura Kakinde, anasema kutolewa mikopo kwa wanawake ni jambo jema, lakini ana angalizo katika umuhimu wa usimamizi wake sahihi.

Ana ushauri kwamba, kinamama wanapaswa wasimamiwe vyema katika mwenendo wao wa kijamii na kiuchumi, hata wafanikishwe kupata pesa zitakazowakomboa kimaisha.

Mshiriki wa mjadala kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Veronica Meaipole, anataja haja ya bima kwa kila mtu ni njema, lakini ikiwa na maelezo ya kina kuhusu matibabu husika yatakavyotolewa.

AFYA

MAMBO YA JKCI...

# Prof. Janabi: Haya ndio mapinduzi namna tunavyotibu umeme moyo

- Ubia na mabingwa nje umejibu
- Mashine ya kisasa imefungwa
- Cha ughaibuni, rasmi nyumbani




Madaktari wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, walipokuwa kazini. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

**Na Christina Mwakangale**

WATAALUMA wa tiba ya moyo wanasema tathmini yao ya jumla, ni kwamba kati ya wagonjwa 100 wanaopatikana na tatizo la mfumo wa umeme wa moyo, 10 wana uwezekano kupata kiharusi, au hata kupoteza maisha.

Imekuwa kawaida baadhi yao wanaofanikiwa kupatiwa tiba, ikiwamo kuwekewa betri au 'pacemaker' ambacho ni kifaa maalum kwa ajili ya kusimamia mtiririko wa mapigo ya moyo.

Mabingwa wa tiba wa maradhi ya moyo wanasema, mapigo ya moyo ya binadamu ni kati ya 60 hadi 100 kwa dakika. Iwapo kunakuwapo chini ya hapo, mtu anapoteza fahamu kila mara, kwa kuwa moyo unavyosukuma damu kwenda mbele hauendani na mapigo ya moyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Prof. Mohamed Janabi, akizungumza kwenye kambi maalum ya siku mbili ya matibabu ya umeme wa moyo, iliyofanyika siku chache zilizopita katika hospitali hiyo, tatizo la mfumo huo huwakumba wenye umri kuanzia miaka 45 hadi 60 au zaidi.

Prof. Janabi anafafanua kuwa wapo wanaozaliwa na tatizo hilo wakirithi na wapo wasiopata kutokana na hitilafu tofauti, kama vile ugonjwa na kufungwa mitambo mipya ya tiba, kumesababisha kupunguzwa rufani za kupeleka wagonjwa nje ya nchi.

Bingwa huyo wa kitabibu, anasema kwa JKCI gharama za matibabu hayo ni kati ya Sh. milioni nne hadi sita kwa mgonjwa mmoja. Anaendelea: "Awali matibabu ya nje yalikuwa kati ya Sh. Mil. 32 (sawa na asilimia12.5 hadi 18.75 ya JKCI) hadi Sh. milioni 35 (asilimia 11.4 hadi 17.2 ya JKCI) baada ya JKCI kuwa na mtambo huu, hatua ya uchunguzi yaani kugundua hadi tiba ni Sh. milioni sita."

### HALI IKOJE?

Prof. Janabi anasema kuna sura tatu za namna ugonjwa huo unavyopatikana, akizitaja kuwa ni maradhi ya presha, umri mkubwa na wengine huzaliwa nayo.

Namna wanavyotibiwa wagonjwa, baadhi ni kwa kutumia mfumo huo au kuwekewa kifaa kiitwacho 'pacemaker' kinachowekwa kifuani kwa mgonjwa kusimamia kasi sahihi za mapigo ya moyo.

"Kwa siku huduma hii katika kambi hii ni kwa wagonjwa wawili, kwa kuwa mgonjwa mmoja na huchukua saa sita kutibiwa kwenye chumba maalum cha tiba ya mfumo wa umeme," anasema.

Ni aina ya utaratibu wa kila mwaka, unatokana na ushirikiano na mabingwa wenzao kutoka nchi tofauti. Prof. Janabi, anaendelea: "Ushirikiano na wenzetu kutoka nje ni kujifunza au kupata uzoefu. Kambi hii imehusisha bingwa kutoka Misri, kutoka hospitali kubwa Afrika kwenye tiba ya mfumo huu.

Anaeleza tiba zilizofanyika ni wagonjwa waliofika kambini ni pamoja na kutimia,

mfumo wa tundu dogo kwa saa mbili, hadi kwenye moyo kufanya ukaguzi kisha kutambua eneo linalotoa umeme mwingi wa moyo na kuunguzwa kwa vifaa maalum.

"Ni kama nyumbani usipokuwa na 'socket breaker' utaunguza kila kitu, kwa umeme mwingi kwenye moyo ni hivyo hivyo. Tiba hii mgonjwa hazimishwi anakuwa na fahamu zake.

"Tunaboresha ujuzi wetu na wenzetu, faida ya kuwaita ni kufundisha madaktari wengi kwa pamoja kwenye mazingira ya vifaa vyetu. Vifaa hivi vina kiwango cha kimataifa, kwa Afrika Mashariki JKCI ni ya pili kuwa navyo, nyingine iliyofungwa mtambo kama huu ni Aga Khan Mombasa, Kenya" anasema Prof. Janabi.

Anasema mashine hiyo ya kibingwa itasaidia wagonjwa wanaohitaji kuwekewa betri (pacemaker) kutohitaji, badala yake wakafanyiwa tiba hiyo kwa kutumia mtambo huo.

"Tulipewa pesa mwaka jana na JPM alitupa Sh. bilioni 4.6 kununua mitambo miwili, hivyo tunaishukuru serikali. Tunaahidi tutatoa tiba kwa wagonjwa, wito kwa madaktari mikoani wakigundua wenye tatizo la mfumo wa umeme wawalete JKC.

"Tiba ni ghali hivi sasa tunaongea na NHIF kuingiza tiba hii kwenye mfumo wao wa huduma," anaongeza bingwa huyo.

### UMEME WA MOYO NI UPI?

Bingwa wa Moyo na Tiba ya Mfumo wa Moyo, JKCI, Dk. Yona Gandye anasema moyo kwa hali ya kawaida hujisisimua wenyewe katika mfumo wake kitaalamu huitwa 'electrical activity' yaani mfumo wa umeme.

"Moyo hufanya kazi wenyewe kwa kufanya uzalishaji wa umeme kwa uaminifu mkubwa sana. Kwa dakika moja huweza kuzalisha mapigo kati ya 60 hadi 100 ambayo ni kawaida.

"Sasa kukiwa na tatizo lolote ikiwa ni la kuzaliwa au la kupata ukubwani kutokana na athari za magonjwa hufanya mapigo kubadilika," anasema Dk. Gandye.

Anasema mfumo wa umeme usio wa kawaida hubadilika kutokana na hitilafu au ugonjwa na kufanya mapigo kuwa chini ya kiwango au juu kupindukia.

Dk. Gandye anasema sababu za tatizo la mfumo wa umeme zipo kwenye makundi kadhaa: Kuzaliwa, kurithi au hitilafu ya mfumo aliyo nao.

Anataja namna anavyopata shida kwa moyo unaotanuka, presha, mishipa mikubwa na kasi ya moyo kupindukia.

### DALILI NA ATHARI

Dk. Gandye anasema kuna wagonjwa wanaokuwa na dalili za kuchoka, moyo kwenda kasi au kupoteza fahamu na kuzinduka.

Anasema, wapo baadhi wanaoonekana kuwafanya waishi kwa muda mrefu bila ya tatizo, ingawa huanguka ghafla na kufariki papo hapo, wakiwamo wanamichezo viwanjani.

"Utakuta hawakuwa na taarifa za ugonjwa wao wa mfumo wa umeme kucheza mpira, labda kukasababisha moyo kutosukuma damu vizuri.

"Pia, wengine hukosa pumzi kutokana na moyo kushindwa kufanya kazi, kutolala usiku au miguu kuvimba ni dalili mojawapo. Uchunguzi husaidia kubaini tatizo, kwa sababu kuna wengine dalili tunazikuta akishafariki," anabainisha Dk. Gandye.

### NENO LA USHUHUDA

Kwenye kambi hiyo wagonjwa sita walitibiwa kutibu mfumo huo na Dk. Gandye anasema, kuliongezeka mtambo mkubwa wa tiba, inayoongeza utoaji huduma ipasavyo, akihimiza Watanzania kufanya uchunguzi wa afya zao mapema.

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo, Prof. Mervat Aboulmaaty, ambaye ni Rais wa asasi yao, The Egyptian Cardiac Rhythm Association (ECRA), anasema amefanya kazi za ushirikiano kama huo, kwa nchi za Kiafrika, ikiwamo, Angola, Sudan, Nigeria na Kenya.

"Nimefurahi kuwa Tanzania, imejikita katika tiba ya mfumo wa umeme na hii inasaidia kupokea maisha. Unaweza kutibu kwa mashine hii na tunashukuru Afrika kuwa na tiba hii," anasema Prof. Mervat.

Anasema alifika nchini Septemba mwaka jana pasipo mashine na anashangaa hatua iliyopigwa kuwapo kifaa hicho, alichotumia kutibu na wenzake wa JKCI.

Bingwa wa kutibu moyo kutoka JKCI, Dk. Honoratha Maucky, anasema kambi hiyo ya wagonjwa wa mfumo huo inapaswa kuwa endelevu, kusaidia wataalamu kujijengea uzoefu.

MAZINGIRA

# Ofisa Mazingira alia kasi uchafu inatisha katika Jiji la Mwanza

## • Kisa; biashara, tabia, kupanuka mji
## • Mto Mirongo hadi Victoria...kinyaa

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

MWANZA ni jiji kubwa kitaifa, katika orodha nyuma ya Dar es Salaam. Kasi yake kukua kiuchumi na kibiashara, iko juu, kupitia ushuhuda wa uwekezaji utokao ndani na nje ya nchi, Vikiwamo viwanda vikubwa na vidogo.

Hapo kwa kina, sekta ya uvuvi itokanayo na Ziwa Victoria na kuliongezea pato la jiji hilo. Lakini kutoka usemi 'kizuri hakikosi kasoro' shida kuu inashuhudiwa kasi kubwa inayoenda sambamba katika uchafuzi wa mazingira.

Adha wakazi kutupa taka ovyo miferejini mtoni, ukiwamo Mirongo na Ziwa Victoria, ikiwa sambamba na ongezeko la wakazi sehemu kubwa wafanyabiashara watokao Kanda ya Ziwa, vyote jumla yake vyaangukia kilio.



Ofisa Mazingira wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Fanuel Kasenene, akikusanya taka kutoka Mto Mirongo.**PICHA ZOTE: ANTHONY GERVA**

**CHANZO NA MADHARA**

Ofisa Mazingira wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Fanuel Kasenene, anabainisha chanzo za uchafuzi huo ni wananchi, akiwa na ufafanuzi:

"Chanzo cha uchafuzi wa mazingira katika jiji hili ni wananchi wanaoishi kando kando ya Mto Mirongo kugeuza mto huo dampo la kutupia taka," anasema.

Kasenene anayataja kasi kuibuka viwanda vikubwa na vidogo, wafanyabiashara wa samaki nchini na kwingineko Afrika. Anaendelea:

" Pia, magulio pamoja na biashara holela kwenye maeneo yasiyokuwa yametengwa rasmi kwa biashara."

Ofisa Mazingira huyo wa Jiji Mwanza, anasema kuna wafanyabiashara wakubwa na wadogo, 500,000 ambao kila siku wanachangia uchafuzi wa mazingira jijini, pia, wenzao katika idadi kama yao kutoka mikoa mingine ya Kanda ya Ziwa wanaoingiza bidhaa na kusababisha uchufuzi wa mazingira.

Kasenene anatahadharisha hatari ya kimazingira, kuibuka magonjwa hatari kama ya kuhara kwa wananchi watumiaji maji ya Ziwa Victoria, ambao kimsingi unapokea kutoka vyanzo mbalimbali, ukiwamo mto mkubwa Mirongo.

Ni muda mrefu, Mto Mirongo umekuwa ukichafuliwa kwa taka hizo, jambo ambalo mtaalam huyo wa afya mazingira, anaeleleza inahatarisha mazalia ya samaki ziwani, pia kuzalisha magugu ya maji.

Anazitaja taka zinazotupwa na wananchi ni pamoja na chupa za maji zilizojazwa mikojo, vifungashio mbalimbali vya bidhaa, mifuko iliyowekewa vinyesi na plastiki mbalimbali zinazozalishwa.

Ukaguzi wa Nipashe, ulishuhudia chupa nyingi za plastiki za maji zilizoelea ufukweni mwa Ziwa Victoria, hali inayotajwa hatari kwa maisha ya wakazi wake.

Ni mandhari hasi inayolikabili jiji la Mwanza, huku kukiwapo vivutio vingi kama vya Hifadhi ya Taifa ya Sanane ndani ya Kisiwa cha Saanane, pia miteremko na kingo za milimailioyosheheni nyumba za wakazi, hata ikageuka kivutio aina yake kwa wageni wafikao ndani ya jiji.

**HATUA INAYOCHUKULIWA**

Kama methali ya Kiingereza inavyotamka 'hakuna jiwe litakaloachwa pasipo kupinduliwa' naye Kasenene anasema, serikali ya mkoa Mwanza imeamua kuleta madaili ya ubora wa mazingira jijini.

Anazitaja hatua zinazojumuisha kupita ndani ya mitaa ya halmashauri kukagua na kutoa elimu ya kuhifadhi taka na mazingira, kila kaya kuwa na chombo maalum na zinasafirishwa kwenda kwenye mahali mahsusi pa kuzihifadhi.

Ni hatua ambayo Kasenene anakiri ni aina fulani ya mtihani kwao, kunakuwapo magumu ya wananchi kutofuata taratibu na sheria za usafi wa mazingira.

Halmashauri ya Jiji imeunda kamati za kusimamia usafi katika mitaa na kata, zinazoelimisha, kujali na kutii kanuni za mazingira kwa manufaa yao na um a klqwa jumla.

Kwa mujibu wa Kasenene, hadi sasa kuna jumla ya magari 13 yanayofanya kazi ya kukusanya taka kutoka vituo 25 na baadaye zinapelekwa katika dampo kuu la kutupia uchafu huo katika eneo analolitaja ni Buhongwa, wilayani Nyamagana.

**SURA YA UCHAFUZI**

Ofisa huyo anabainisha, kwamba ipo sheria ndogo ya kuhifadhi mazingira na sheria mama inayomtaka mtu au kaya inayozalisha taka kuhifadhi kwenye chombo maalum cha kuhifadhia na siyo kutupa ovyo.

Anasema, Halmashauri ya jiji la Mwanza limeweka mfumo maalum wa wakala wanaofanya kazi ya kukusanya taka hizo mitaani na kuzipeleka kwenye vituo rasmi vilivyowekwa, ili baadaye zipelekwe iliko dampo kuu.

Kasenene anasema, sheria inamhitaji kila mzalishaji taka, azingatie taratibu za usafi na kulipa gharama ya Sh.5, 000 kila mwezi kwa ajili ya kuwahudumia wakusanyaji taka na anasema kwa wanaoishi kwenye makazi ya ngazi za juu wanalipa Sh.15, 000 kila mwezi za usafi wa mazingira.

Sheria inataja faini kwa wakosefu katika uchafuaji mazingira, wakitozwa faini zinazoanza Sh. 300,000 hadi Sh. milioni 50 kulingana na kiwango cha uchafuzi, ikiwamo ngazi ya juu viwandani.

Kasenene anataja mitaa inayoongoza kwa uchafuzi wa mazingira jijini Mwanza ni Lumumba, Pamba na Rwagasorwe, ambayo kimsingi ina wafanyabiashara wengi wakubwa na wadogo.

Namna ya kufanikisha hilo, anasema tayari Halmashauri ya Jiji Mwanza imeajiri jumla ya watu 500 wa kufanya usafi huo wa mazingira katika mitaa yote jijini.

Kasenene anasema, hadi sasa kinachomkera zaidi katika kazi yake, ni tabia ya makada na hulka tofauti walizo nazo kutojali usafi wa mazingira na hasa utupaji taka ovyo.

"Kitu ambacho ni 'pasua kichwa' na kinanisumbua nikiwa kazini, ni tabia za watu wengi katika makabila yao hupenda kuishi na uchafu hata majumbani mwao, bila kujali usafi wakiona ni jambo la kawaida,' analalamika Ofisa Mazingira Kasenene.

Maelekezo yake akiwa amebeba rungu la kimamlaka ni kwamba, wakazi wa jijini Mwanza wabadilike kitabia, kwani vinginevyo sheria itachukua mkondo wake, kuwakamata na kuwaadhibu, kulingana na sheria zilizopo.

Kimsingi, itaendelea kupita mitaani kukagua usafi wa mazingira,ikiwamo kuwatoza faini ndogo za Sh,50,000 wananchi wanaotupa taka ovyo kwenye maeneo yasikuwa rasmi kuhifadhi taka zao.

Anabainisha licha ya hivyo watahakikisha wanatoa elimu kupitia vyombo vya matangazo mtaani, mikutano ya hadhara ya wananchi pamoja na kufanya kampeni za usafi kila mwezi, ili kuboresha huduma hiyo kwa wananchi wake.



Taka zilizokusanywa, ili kudhibitiwa ziingie katika Ziwa Victoria, kuhatarisha mazalia ya samaki na kuzalisha magugu maji kwa wingi. Chupa nyingi zimehifadhi uchafu wa binadamu.

AFYA

## MAGEUZI YA DEMOGRAFIA

# Kudhibiti uzazi China kunavyomaliza idadi vijana, watoto, nguvukazi taifa




Wachina wakiwa katika mkusanyiko unaowahusu. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Christina Mwakangale**

KATI ya watu bilioni 7.7 wanaokadiriwa kuwapo duniani, wapo bilioni 1.4 sawa na asilimia 18 ya idadi hiyo ni Wachina, kwa mujibu wa takwimu za idadi ya watu wa Idara ya Kiuchumi na Kijamii ya Umoja wa Mataifa (DESA), mwaka 2019

Umati wa Wachina hao unafuatiwa kwa karibu na Wahindi walioko bilioni 1.38 sawa na asilimia 17.9 ya wakazi wa duniani. Kwa maana hiyo, theluthi moja ya wakazi duniani sawa asilimia 35.9 wako katika nchi hizo mbili, China na India.

Wachina hao wana sifa ya ziada, kwamba kundi la wazee ni wengi zaidi na vijana. Ni hali inayoendana na kuzaliwa watoto kidogo, sababu kuu ni mpango wa nchi hiyo na sheria kali zilizowekwa awali kukabiliana na idadi ya watu.

### TAIFA LINAVYOTIKISWA

Hali hiyo inatajwa kutishia mustakabali wa taifa la China, lenye ushawishi na mafanikio duniani, ikizingatiwa kuna idadi ndogo ya nguvu kazi, ambayo ni vijana.

Chama tawala cha Kikomunisti kilianza kuchukua hatua mwaka 2015 na kulegeza sharti la kuzaa mtoto mmoja, hadi kutolewa ruksa ya kuzaa watoto wawili.

Viongozi nchini humo wameeleza namna hali hiyo inavyowapa changamoto kwa kuwa, idadi ya umri wa watu wanaotakiwa kufanya kazi inaporomoka kila uchao, kulingana takwimu ya sensa iliyotolewa Jumanne wiki iliyopita na kutangazwa katika vyombo vya habari vya kimataifa.

Sensa hiyo inafafanua China hadi sasa ina wananchi bilioni 1.411. Hisabati iliyopo ni kwamba kulikuwapo ongezeko la watu milioni 72 katika kipindi kutoka mwaka 2010.

Takwimu ya sensa nchini humo hufanyika kila baada ya miaka 10. Sababu ya kuwapo watoto wachache, wengi walio kwenye uhusiano, ndoa au wenzi, hawako tayari kuzaa.

Viongozi wanasema wakati kuna mkakati wa kukuza jamii yenye utajiri na dunia kutambua kama taifa linalokua kwa kasi kiuchumi kupitia viwanda, teknolojia na kujitegemea, changamoto inayowakabili ni nguvu kazi

Chama kinachoongoza taifa hilo tangu mwaka 1980, waliweka ukomo wa idadi ya watoto kuzaliwa kwa kila familia, ili kukabili wingi wao, ingawa hadi sasa kunashuhudiwa kudidimia idadi hiyo ya nguvu kazi.

Masharti hayo yalilegezwa baadae, ingawa bado wengi hawazai watoto wakidai kwamba gharama za malezi ni kubwa, makazi duni na kuwapo ubaguzi katika ajira dhidi ya kinamama.

Idadi ya wafanyakazi wazalishaji wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 59 iliporomoka na kufikia milioni 894, mwaka jana, kwa mujibu wa Kituo cha Taifa cha Takwimu China ni sawa na theluthi mbili ya Wachina wote (63.8%).

Inaelezwa, wazee walio na umri kuanzia miaka 60 na zaidi wanaongezeka kwa kasi kuliko watoto, hali ambayo ni mabadiliko zamani watoto ndio waliongezeka.

Ning Jizhe, Mkurugenzi wa kituo hicho anasema mwaka jana walizaliwa watoto milioni 12. Hata hivyo, mwaka juzi 2019 walizaliwa watoto milioni 14.6.

### KUYUMBA DEMOGRAFIA

Wataalamu duniani wanasema, China, Thailand na nchi nyinginezo zinazoendelea za bara Asia zinakabiliwa na tatizo la kasi ya maendeleo isiyowiana na idadi ya watu ambao ongezeko lake linasuasua.

Wachumi wanaionya China kwamba idadi hiyo isiyoendana kidemografia ni bomu linalokuja na Rais wa China, Xi Jinping, anasema bajeti kubwa inayotumiwa na serikali kuimarisha jeshi na kujenga ushindani kimataifa ni kubwa, hivyo kunahitajika mafanikio kwenye ukusanyaji mapato na uchumi ili kutekeleza hayo.

"Tuna wasiwasi zaidi juu ya kupungua kwa kasi kwa idadi ya watu wanaofanya kazi, ikilinganishwa na idadi ya watu wote," anachangia Prof. Lu Jiehua, mwanazuoni katika stadi ya idadi ya watu.

Msomi huyo anasema, mabadiliko hayo ya kupungua nguvu kazi iliyoanza kujionyesha miaka 10 iliyopita, kuna shaka hadi kufika mwaka 2050 kutakuwapo uhaba mkubwa wa nguvu kazsju ndani ya China.

"Kama idadi ya watu ni ya wazee zaidi, itakuwa ngumu kutatua matatizo ya Uhamiaji. Tutatue mapema suala hili," anasema Prof. Lu Jiehua.

### KWANINI WENGI HAWAZAI?

Takwimu za utafiti nchini humo, zinasema, wenzi wengi hawazai watoto kutokana na matatizo mengi, ikiwamo makazi wengi wakiishi nyumba moja na wazazi wao.

Pia, kunadaiwa kuwapo siku chache za likizo ya uzazi; na kinamama wengi wanalea pekee na hawamo kwenye mfumo rasmi wa huduma za afya na malipo ya ulezi.

Lingine kutajwa ni kuwapo kinamama wanaohofia kuzaa kwamba, huenda vipaji vyao vitaathiriwa.

"Ukiwa na mtoto unapata likizo ya uzazi, lakini kazi itakuwa nayo baada ya kumaliza likizo hii, hofu ni hii," anasema, He Yiwei, mwanamama ambaye muda mfupi aliyerejea China, kutoka masomoni Marekani, kupata shahada yake ya pili.

Mataifa kama Japan na Ujerumani, nazo zina magumu ya umri na idadi ndogo ya vijana na kwamba mbadala unaweza kuhamishia juhudi zao kuwekeza kwenye viwanda kiteknolojia.

China ni ncbhi iliyowekeza uchumi wake kwenye kilimo na nguvu kazi ya uzalishaji kiteknolojia.

Kupungua kwa idadi ya watu wenye umri wa kufanya kazi kutaweka kikomo cha ukuaji wa uchumi wa China, kunahitajika mageuzi kiuchumi," anasema mtalamu Yue Su wa kitengo cha Intelijensia ya Uchumi.

Shirika la Kimataifa wa Fedha (IMF), linaatabiri uchumi wa China utakua kwa asilimia 8.4 mwaka huu, licha ya kubeba janga la corona.

Chama cha Kikomunisti, kinataja mikakati yake kuanzia mwaka jana ni kuongeza pato mara mbili kwa kila mtu hadi kufikia mwaka 2035. Wastani wa ukuaji pato la kila mtu kwa mwaka ni asilimia 4.7.

### NCHI ILIKOTOKEA

Kihistoria, idadi ya vizazi vya China haiko tofauti sana na nchi za Korea Kusini, Thailand na nyinginezo barani Asia, hata kabla ya amri ya uzazi wa mtoto mmoja.

Benki ya Dunia (WB) inaeleza watoto waliozaliwa China katika miaka ya 1960 walikuwa wastani sita kwa kila mwanamke, lakini hadi kufikia miaka 1980, walishuka hadi watatu.

Sheria ya kuwa na mtoto mmoja pekee, iliendasambamba na adhabu ama kulipa fainia au kupoteza ajira na kutoa ujauzito.

Kipaumbele kilikuwa kwa watoto wa kiume pekee na kusababisha matukio watoto wa kike kuuawa, kupita tafsiri iwapo wanaume watakuwa wengi, watakosa wake wa kuwaoa na kuchochea hamaki kwenye jamii.

Yi Fuxian, mwanasayansi mbobezi katika masuala ya uzazi, kutoka Chuo Kikuu cha Wisconsin-Madison, Marekani anasema idadi ya watu iliporomoka tangu mwaka 2018, huku watunga sera wakitaka kuweka umri rasmi wa kustaafu kuwa miaka 55, ili kuongeza kiwango cha wafanyakazi.

***• Kwa mujibu wa taarifa za tofauti.***



# Wabunge wataka idara maalum kortini sasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WABUNGE wameshauri kuwapo kwa idara maalum katika mahakama za mwanzo nchini ambazo zitafanya kazi ya kushughulika na migogoro ya ardhi ili kukomesha tabia za baadhi ya watu kutoheshimu uamuzi unaotolewa na mabaraza ya ardhi nchini.

Ushauri huo waliutoa jana kwenye mafunzo ya uandaaji wa bajeti inayozingatia usawa wa kijinsia iliyotolewa na Shirika la Kimataifa la Care kwa kushirikiana na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) wakishirikisha Umoja wa Wabunge Wanawake (TWPG).

Akizungumza katika mafunzo hayo, Mbunge wa Nyasa (CCM), Stella Manyanya, alisema kuna umuhimu wa serikali sasa kuanzisha idara maalum inayohusika na kesi za ardhi katika mahakama za mwanzo nchini ili kutatua migogoro hiyo.

Alisema watu ambao mashauri yao yanakuwa yameamuliwa na mabaraza hayo wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa na kuchukua muda mrefu kutekelezwa.

"Kuwe na department (idara) maalum katika mahakama inayoshughulika na migogoro ya ardhi, ziende hadi katika mahakama ya mwanzo. "Kwa sababu bado inaonekana kuwa kuna wadau wengine hawaheshimu uamuzi wa haya mabaraza ya ardhi," alisema Manyanya.

Mbunge wa Sikonge (CCM), Joseph Kakunda, aliwataka wabunge kuwasaidia mawaziri wa ardhi katika kuhakikisha kuwa serikali inapanga bajeti itakayowezesha kupima vijiji na kuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Alisema zinahitajika Sh. bilioni 180 kwa ajili ya kupima ardhi ya vijiji zaidi ya 12,000 vilivyopo nchini.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, alisema kuanzia Februari mwaka huu hukumu zote zinaandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Alisema kuwa moja ya matatizo ambayo yalikuwa yakiwakabili wananchi wa hali ya chini ni hukumu zinatolewa kwenye mabaraza ya ardhi kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

Alisema hivi sasa serikali tayari imetoa mwongozi wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za mabaraza hayo ikiwamo utoaji wa hukumu kutumia lugha hiyo.



Mbunge wa Same Mashariki, Anne Kilango Malecela, akiuliza swali kwenye vikao vya Bunge la Bajeti vinavyoendelea, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TRA yanyooshea kidole uadilifu wa watumishi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Mapato (TRA), imesema baadhi ya watumishi wasio waadilifu wanasababisha upotevu wa mapato na kusababisha serikali kutofikia malengo.

Kufuatia hali hiyo, imejipanga kutekeleza ipasavyo mkakati wa miaka mitano wa taifa dhidi ya rushwa awamu ya tatu (NASCAP III) wenye lengo la kudhibiti vitendo vya rushwa vinavyofanywa na watumishi hao.

Akifungua warsha ya kutathimini utekelezaji wa mpango huo juzi jijini hapa, Naibu Kamishna Mkuu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudhibiti Uadilifu ya Menejimenti ya TRA, Msafiri Mbibo, alisema ili kutekeleza mkakati huo kila idara katika mamlaka hiyo iliainisha maeneo yenye viashiria vya rushwa na kuandaa mikakati ya namna ya kushughulikia kupitia kamati za kudhibiti uadilifu.

"Rushwa ni moja ya changamoto zinazoikabili taasisi mbalimbali ikiwamo Mamlaka ya Mapato, vitendo vya rushwa vinavyofanywa baadhi ya watumishi wasio waadilifu vinasababisha upotevu wa mapato na kukwamisha lengo la serikali la kuwahudumia Watanzania," alisema.

Naibu kamishna huyo alisema kupitia warsha hiyo watafanya tathmini ya ufanisi wa utekelezaji tangu ulipoanza mwaka 2017, lengo likiwa kuangalia mafanikio, vikwazo na kupendekeza maboresho ili kutimiza malengo ya mkakati.

Awali, Mkurugenzi wa Idara ya Mambo ya Ndani ya TRA, Ndositwe Haonga, alisema mkakati huo ulianzishwa na serikali mwaka 2017 na unatarajia kukamilika mwaka 2022.

Alisema mapendekezo yatakayopatikana kwenye warsha hiyo yatasaidia mamlaka kupitia Idara ya Mambo ya Ndani kuboresha mkakati na kupanga mipango mizuri ya kukabiliana na rushwa na ukiukwaji mwingine wa maadili katika ukusanyaji wa kodi.

# 'Chakula huua watu 420,000 kila mwaka'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WATU 420,000 hufariki dunia kila mwaka kutokana na kula chakula ambacho si salama kwa afya ya binadamu.

Akitoa mada kwenye semina ya waandishi wa habari kuhusu athari za sumukuvu, Mwanaidi Kiya, ofisa wa Wizara ya Kilimo, alisema juzi kuwa idadi hiyo ni kubwa na nguvu kazi inapotea.

Alisema fedha nyingi pia zinapotea kwa ajili ya matibabu ya watu walioathirika.

"Hali ya udhibiti wa ubora wa chakula ili kisichafuliwe inapaswa kuongezeka kwa kiasi kikubwa ili kukabiliana na suala hili ambalo serikali inapambana kuhakikisha

hakuna tatizo la sumukuvu ambalo linatokea au kuendelea katika mikoa ambayo ilishawahi kukumbwa na kadhia hiyo," alisema.

Aliwataka waandishi wa habari kuhakikisha wanaelimisha jamii kuhusu suala la sumukuvu ili

kudhibiti tatizo hilo wakati wa mavuno.

Mratibu wa mradi wa kudhibiti sumukuvu, Josephat Crepin, alisema mradi huo umelenga kudhibiti na kutoa elimu juu ya tatizo la sumukuvu.

Josephat alisema waandishi wa habari wanapaswa kutumia kalamu zao kutoa elimu ya kukabiliana na tatizo hilo.

"Ninaiomba jamii isiwe na wasiwasi kuhusiana na sumukuvu, Wizara ya Kilimo pamoja na taasisi zinazohusiana na masuala ya chakula zipo mstari wa mbele kukabiliana na changamoto hiyo," alisema Josephat.

Awali, akifungua semina hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Usalama na Chakula, Josephine Amori, alisema wizara imejipanga kuweka mikakati ya kukabiliana na sumukuvu kwa kuanza ujenzi wa miundombinu sahihi ya kuhifadhi mazao na kutoa elimu kwa wakulima na wasindikaji.

Alibainisha tatizo hilo si Tanzania pekee bali linazikabili nchi nyingi na husababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Alitaja mazao yanayoathiriwa na sumukuvu kuwa ni mahindi na karanga na kuitaka jamii kufuata utaratibu sahihi wakati wa kupanda na kuhifadhi mazao hayo.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Wizara hiyo, Revocatus Kasimba, aliwataka wanahabari kwenda kuielimisha jamii

kuhusiana na suala la kudhibiti sumukuvu tangu mazao yakiwa shambani hadi kwenye kuhifadhiwa.





# Maporomoko yaua, kuharibu makazi

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

MTU mmoja amefariki dunia na kaya zaidi ya 30 hazina makazi, baada ya nyumba zao kufunikwa na udongo ambao umeporomoka kutoka milimani.

Hali hiyo imetokana na mvua kubwa iliyonyesha katika Bonde la Mwakaleli, Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe.

Mvua hiyo pia imesababisha mafuriko yaliyoharibu zaidi ya ekari 50 za mazao, kuvunja madaraja na mawasiliano ya barabara mbalimbali kukatika baada ya kusombwa na maji.

Gazeti hili lilifika katika Bonde la Mwakaleli na kushuhudia nyumba za wananchi zikiwa zimevunjika, baada ya kufunikwa na udongo, huku mazao mengi hasa migomba ikiwa imesombwa na maji.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ikubo kilichopo Kata ya Luteba, Mwakahoji Mwaisabila, alisema katika kijiji chake mtu mmoja alifariki dunia, baada ya udongo ulioporomoka kutoka mlimani wakati mvua hiyo ikinyesha kufunika nyumba yake wakati yeye akiwa amelala.

"Kwenye kijiji changu ni mtu mmoja aliyekufa, mtu huyo alifariki kwa sababu wakati mvua inanyesha na udongo unaporomoka kutoka mlimani yeye alikuwa amelala na nyumba hiyo ikafunikwa na udongo huku yeye akiwa ndani amelala," alisema Mwaisabila.

Alisema mbali na kifo hicho, pia Mto Sokolo unakatisha kijijini hapo uliacha njia yake ya kawaida, ukavamia mashamba ya wananchi na kusababisha uharibifu mkubwa.

"Mahamba yetu mengi yameharibiwa na maji ya Mto Sokolo baada ya mto huo kuacha njia na kupita kwenye mashamba yetu, mazao yetu kama vile migomba, magimbi, viazi na mengine mengi yameharibiwa," alisema Mwaisabila.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, alisema madhara ya mvua hiyo ndani ya wilaya yake ni makubwa kwani zaidi ya nyumba 30 zilizolewa na kusababisha wananchi kukosa makazi.

Aidha, Chalya alisema kuwa mvua hiyo pia iliharibu miundombinu ya barabara ambapo kuna madaraja zaidi ya manne yamevunjika na maeneo mengine barabara zilifunikwa na udongo uliokuwa ukiporomoka kutoka milimani kiasi cha kutopitika kabisa.

"Tumeumia sana baada ya kupata taarifa za kifo cha kijana wetu Mpoki ambaye alifunikwa na udongo akiwa amelala ndani ya nyumba, lakini kubwa ni kwamba pamoja na familia hii kumpoteza mpendwa wao. Pia kuna kaya 20 katika kata ya Luteba lakini kuna familia tano ziko ndani ya Kisiba na nyingine nyingi ndani ya Wilaya ya Rungwe hazina makazi kutokana na mvua hiyo kuvunja nyumba zao," alisema Chalya.

Chalya aliwataka wananchi walio jenga kwenye mikondo ya maji kuanza kuondoka kwenye maeneo hayo ambayo ni hatarishi kwa maisha yao.

Alisema yeye baada ya kupata taarifa za maafa hayo, aliwasiliana na Mbunge wa Busokelo na kumwomba afikishe taarifa hizo Serikali Kuu kwa vile wakati huo mbunge huyo alikuwa Dodoma ambako anahudhuria vikao vya Bunge la Bajeti.

Alisema serikali ilipopata taarifa imetoa misaada ya awali ya kibinadamu kwa wananchi hao na kumtumba Mbunge Mwakibete kuileta kwa wananchi.

Mbunge Mwakibete alisema serikali ilipopata taarifa ya maafa hayo ilimtuma kuwapatia pole wananchi sambamba na kumpatia vitu mbalimbali kuwaletea kama msaada wa awali wa kibinadamu.

Mwakibete alivitaja baadhi ya vitu hivyo alivyopewa ni ndoo 100 za lita 10, ndoo 80 za lita 20, mikeka 500, madumu ya maji 200, masufuria 200, magodoro 30 na mablanketi 56 pamoja na fedha kidogo kwa ajili ya rambirambi kwenye familia iliyofiwa.

"Serikali inayoongozwa na Rais wetu Samia Suluhu Hassan na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia kitengo cha maafa wamenituma niwapatie pole sana, lakini wameniambia kuwa serikali haijawaacha bure na hivyo wamenipatia vitu hivyo niwaletee," alisema Mwakibete.

Kuhusu uharibifu uliojitokeza kwenye miundombinu ya barabara, Mwakibete alisema serikali imefanya mazungumzo na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kuweka daraja la chuma kwenye Mto Ikubo ambalo ni kiunganishi muhimu ndani ya bonde la Mwakaleli ili shughuli za kiuchumi na kijamii ziendelee.

Alisema miundombinu mingine ya barabara itaendelewa kufanyiwa marekebisho taratibu na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) mpaka hali ya miundombinu hiyo itakaporejea katika hali yake ya kawaida.

## Matatani tuhuma za mauaji ya mwanachuo

**NA Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linamshikilia kijana mmoja, Oscar Mwasomi (18), ambaye ni mfanyabiashara na mkazi wa Maanga jijini Mbeya kwa tuhuma za mauaji ya mwanafunzi wa Chuo cha Biashara (CBE) Tawi la Mbeya, Geoffrey Nyoni (20).

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema tukio hilo lilitokea Mei 17, mwaka huu saa 5:00 usiku.

Alisema Mwasomi akiwa na wenzake wanne akiwamo mmoja ambaye alijulikana kwa jina moja la Madenge walimshambulia mwanafunzi huyo na kumpiga na vitu butu maeneo mbalimbali ya mwili wake, hali ambayo ilisababisha kifo chake.

Kamanda Matei alisema chanzo cha tukio hilo ni watuhumiwa kumtuhumu mwanafunzi huyo kuiba simu na nguo za Madenge ambaye walikuwa wamepanga kwenye nyumba moja na kwamba baada ya tukio hilo watuhumiwa wengine walitokomea kusikojulikana.

"Tunaendelea na msako mkali wa kuwatafuta watuhumiwa wengine ambao walitoroka baada ya kutekeleza tukio hilo, wakipatikana watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani," alisema Kamanda Matei.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi kwa maelezo kuwa ni kunyume na sheria na hivyo akawataka kusuluhisha matatizo yao kwa kufuata sheria za nchi.

Katika tukio lingine Kamanda Matei alisema jeshi hilo linawashikilia watu watatu wakazi wa Wilaya ya Kyela kwa tuhuma za kukutwa na dawa za kulevya aina ya Heroine kete saba.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Victor Patrick (45), Daniel Ndunguru (38) na Allen Alfan (41) wote wakazi wa Wilaya hiyo ya Kyela ambao walikamatwa wakiwa na dawa hizo haramu.

Alisema watuhumiwa walikamatwa Mei 17, mwaka huu majira ya saa 9:20 alasiri Mtaa wa Uwanja wa Siasa uliopo Kata ya Mbugani wilayani humo.

Alisema watu hao walikutwa ndani ya moja ya nyumba za eneo hilo wakiwa wanatumia dawa hizo za kulevya, na kwamba watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi wa tukio hilo kukamilika.



Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya ABSA Tanzania, Obedi Laiser (kushoto), akishikana mikono na Mkuu wa Huduma kwa Wateja na Digitali wa benki hiyo, Samuel Mkuyu, wakati wa uzinduzi wa mfumo wa kidigitali unaowezesha upatikanaji wa huduma za kibenki kwa njia ya mtandao wa WhatsApp, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkuu wa Wateja Binafsi wa benki hiyo, Oscar Mwamfwagasi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wajasiriamali wapewa mbinu uandaaji bajeti

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAFANYABIASHARA na wajasiriamali wengi nchini wanashindwa kufikia malengo ya shughuli zao, kutokana na kutokuwa na utaalamu wa namna bora ya upangaji wa bajeti kuanzia ngazi ya familia.

Kukosa elimu ya upangaji bajeti kwa makundi hayo kumechangia kukwamisha ukuaji wa biashara na kushindwa kufikia malengo na kuendelea kulimbikiza madeni na kusababisha msongo wa mawazo.

Mkurugenzi wa Shirika la Elimisha, Festo Sikagonamo, alisema lengo la kuanzishwa kwa shirika hilo ni uwezeshaji vijana na wanawake wasiokuwa na ajira kwa kuwafundisha mbinu za kupata kazi halali zinazolenga kutatua tatizo ili kuwa na maisha bora endelevu na yenye kutimiza ndoto zao kuanzia ngazi ya kaya.

Kutokana na vikwazo mbalimbali vinavyosababishwa na ukosefu wa elimu ya upangaji bajeti kuanzia ngazi ya familia Sikagonamo ameanzisha program ya kuwajengea uwezo wajasiriamali na wafanyabiashara wanawake na vijana umuhimu wa bajeti.

Alisema hadi sasa wafanyabiashara na wajasiriamali zaidi ya 100 wa jijini Mbeya, wamepatiwa elimu ya upangaji bajeti kuanzia ngazi ya familia na kwamba hata taasisi na mashirika ya umma na binafsi wamepatiwa elimu hiyo.

Aliongeza kuwa mbali na kuwapatia elimu ya upangaji bajeti, lakini wamepatiwa elimu ya uongozi kwa wanawake na wanaume ikilenga zaidi kuwahamasisha kugombea kwenye kamati mbalimbali za uongozi wa mtaa au vijiji ambako huko wataweza kuwasilisha kero zao na kutatuliwa.

Mtendaji wa Kata ya Sinde, Hawa Kajula, ambaye alitoa mafunzo ya uongozi kwa wajasiriamali hao, aliwahamasisha kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za kamati ili kupaza sauti zao.

Alisema uongozi bora unaanza kutengenezwa kuanzia ngazi ya chini kwenye mitaa na vijiji na kwamba akiwandaliwa vyema anaweza kuja kiongozi mzuri hapo baadaye.

Mmoja wa wanufaika wa mafunzo hayo, Regina Sanga, alisema kuwa upangaji wa bajeti kuanzia ngazi ya familia ni jambo muhimu katika mafanikio ya nchi na kwa mtu mmoja mmoja.

Sanga ambaye ni mkulima wa mboga na matunda, anasema laiti elimu ya upangaji bajeti angeipata tangu zamani angekuwa mbali kimaendeleo, alisema amekuwa hana bajeti na fedha anayoipata kutokana na biashara ya kuuza mboga lakini kwa sasa atahakikisha anazingatia nidhamu ya matumizi ya fedha anayoipata.

Edna Mwakatobe alisema elimu ya upangaji wa bajeti itamwezesha kuhudumia familia yake vizuri kwa kuhakikisha anatanguliza vipaumbele muhimu ikiwa ni pamoja na kusomesha watoto na kufanya shughuli nyingine za maendeleo.

Ikumbukwe kuwa ili kufikia taifa lenye uchumi wa kijitegemea, elimu ya upangaji wa bajeti kuanzia ngazi ya familia inatajwa kuwa na mchango mkubwa katika kufikia mafanikio hayo.



# Sababu za sheria ya wafungwa kutumikia jamii kukwama hizi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema Sheria Namba 6 ya Mwaka 2018 ya wafungwa wenye vifungo vidogo kutumikia jamii, imekwama utekelezaji wake.

Imesema hali hiyo imetokana na kukosekana kwa maofisa wa ustawi wa jamii wa kutosha kwa ajili ya kasimamia.

Hayo yameelezwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Katiba na Utumishi wa Umma), Haroun Ali Suleiman, alipokuwa akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, katika Baraza la Wawakilishi.


Alisema serikali ilitunga sheria hiyo kwa madhumuni ya kupunguza mrundikano wa wafungwa katika magereza, lakini utekelezaji wa sheria hiyo umekwama kutokana na changamoto zilizojitokeza.

Waziri Haroun alizitaja changamoto hizo ni kutokuwapo kwa wasimamizi wa wafungwa wanaotumikia adhabu, kuwapo kwa askari wa magereza wanaotumikia kazi mbili za kusimamia wafungwa wanaotumikia ndani ya chuo cha mafunzo na wafungwa wanaotumikia jamii.

Aidha, alisema kukosekana kwa maofisa wa ustawii wa jamii wa kuwasimamia pia kumeibua changamoto kubwa ambao wangepaswa kwenda kukagua kazi za wafungwa katika maeneo ya huduma za jamii.

"Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa sheria hii, serikali itachukua hatua za kiutendaji ikiwamo kubainisha wasimamizi wa wafungwa wanaotumikia jamii pamoja na kuwapo kwa maofisa wa jamii wa kutosha wa kukagua kazi za wafungwa wa huduma za jamii," alisema Waziri Haroun. Alisema nia ya serikalini ni kuona sheria hiyo inafanyakazi kwa wafungwa wenye vifungo vidogo chini ya miezi sita ili kuondoa mrundikano wa wafungwa katika magereza visiwani humo.

Awali Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, alitaka kufahamu kwanini Sheria Namba 6 ya Mwaka 2018 inayotoa adhabu kwa wafungwa wenye vifungo vidogo kutumikia jamii imekwama utekelezaji wake tangu kupitishwa na kusainiwa na Rais wa Zanzibar.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhiwa zawadi ya kitabu na Balozi Mdogo wa Jamhuri ya Watu wa China anayefanya kazi zake Zanzibar, Zhang Zhisheng, baada ya kumaliza mazungumzo yao Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Wawakilishi wataka usimamizi wa sheria

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imetakiwa kusimamia sheria ili kudhibiti udhalilishaji wa wanawake na watoto pamoja na uvunjaji wa sheria uliofanywa na Bodi ya Udhibiti Vileo, baada ya kutoa vibali vya uingizaji pombe kwa kampuni 8 badala ya tatu.

Wito huo umetolewa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Mahonda, Asha Abdalla Mussa, Nadir Abulratifu (Chaani), Issa Haji Gavu Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka wakati wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum) katika mkutano wa Tatu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar jana. Nadir alisema Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar imetoa vibali kwa kampuni za uingizaji vileo zaidi ya tatu kinyume cha kifungu cha 33(1) sheria ya vileo lakini wizara imeshindwa kuchukua hatua dhidi ya watendaji waliovunja sheria hiyo.

"Ofisi yako au taasisi yako imetoa leseni za waingizaji pombe zaidi ya sheria tuliyopitisha sisi ndani ya Baraza la Wawakilishi wakati sheria inasema mwisho kampuni tatu, "alisema Bwana Nadir. Aidha, alisema kwamba bado kumbi za disko na baa zimendelea kufanyakazi kama kawaida katika maeneo ya huduma za jamii na makazi ya watu licha ya kuwa kinyume na sheria namba tisa ya udhibiti wa vileo ya mwaka 2020.

Waziri wa zamani wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Issa Haji Gavu, alisema wakati umefika wizara kueleza umetumika utaratibu gani wa kuongeza idadi ya kampuni za uingizaji vileo Zanzibar kinyume cha sheria iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Gavu alisema kwa mujibu wa sheria waziri ndiye msimamizi na yeye ndiye mwenye mamlaka ya kuiongoza na kuelekeza Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar.

"Mheshimiwa Spika, mimi hoja yangu nataka nijue Mheshimiwa Waziri kwenye hili anataka kutueleza vipi je, yeye amekuwa sehemu ya uvunjaji wa sheria hii... sehemu ya kusaidia watu wanaovunja sheria, sipo tayari kuona taasisi ya serikali inakuwa kichocheo cha kuvunja sheria za serikali," alisema Waziri wa Gavu.

Mwakilishi wa Jimbo la Mahonda, Asha Abdallah Mussa, alisema matukio ya udhalilishaji wa wanawake na watoto 1151 yameripotiwa Zanzibar katika kipindi cha Julai hadi Machi mwaka 2020/2021, lakini kesi zilizopatiwa ufumbuzi chache licha ya watuhumiwa kufikishwa polisi.

Asha alisema: "Mheshimiwa Spika, ningemwomba Makamu wa Pili wa Rais afanye ziara maalum katika vituo vya polisi kushughulikia suala zima la kesi za udhalilishaji kwanini zimekwama," alisema Asha na kuibua makofi.

Mjadala mkubwa uliibuka katika mkutano wa bajeti juu ya udhalilishaji wa wanawake na watoto pamoja na Bodi ya Vileo Zanzibar kuvunja sheria, baada ya kuruhusu kampuni zaidi ya nane kuingiza vileo badala ya tatu kinyume cha sheria iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi na kuanza kutumika baada ya kusainiwa na Rais Mei 11, mwaka jana.

# Mabaraza Anglikana yakunwa maridhiano ya kisiasa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mabaraza ya Makanisa ya Anglikana Bara la Afrika (CAPA), Johnson Koffi, amesema nchi za Afrika zinapaswa kuiga mfano wa Zanzibar katika kufikia maridhiano ya kisiasa.

Kwamba maridhiano hayo yamefungua milango ya wananchi na kutoa nafasi ya kufanya shughuli zao kwa amani ikiwamo kuabudu.

Aliyasema hayo wakati akizungumza katika mkutano wa kuimarisha uelewa wa utulivu na utamaduni wa kuheshimiana na kuvumiliana kupitia dini tofauti, uliofanyika Zanzibar, ambao uliwashirisha wadau kutoka nchi za Afrika.

Aliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa kuwa nchi ya kupigiwa mfano katika kuheshimu uhuru wa kuabudu na uvumilivu wa imani za dini tofauti.

"Nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufikia maridhiano ya kisiasa ambayo yamefungua milango ya kuimarisha kwa uhuru wa kuabudu sambamba na uvumilivu wa wafuasi wa dini tofauti kuheshimiana," alisema.

Aidha, alisema Waafrika wanaweza kufurahia maisha bora ndani ya neema kubwa ya utajiri wa rasilimali za asili zilizobarikiwa Afrika kwa kuwa na sauti moja ya maridhiano na kuzifanya imani za kidini kuwa daraja la kuwapandisha, badala ya kuwa kikwazo na kuitolea mfano Zanzibar kuwa nchi ya mfano.

Akifungua mkutano huo, Katibu wa Kamati ya Amani Zanzibar, Sheikh Fadhil Soraga, alisema Zanzibar imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuwaunganisha watu wenye imani tofauti za dini ambapo Waislamu na Wakristo na waumini wengine wamekuwa wakiishi kwa amani na utulivu.

Alisema mradi wa kuhamasisha amani na uvumilivu wa imani za dini kwa kiasi kikubwa umeleta mabadiliko makubwa na kuondoa ubaguzi wa kubaguana kutokana na tofauti za imani, utamaduni na itikadi za kisiasa.


"Mradi wa kuhamasisha amani na kuondosha tofauti za kidini na chuki za kisiasa kwa kiasi kikubwa umesaidia kuwapo kwa maridhiano ya kisiasa kwa viongozi wa vyama vya siasa, hatua ambayo leo hii imefungua maelewano na kuwapo kwa utulivu mkubwa," alisema.

Naye Naibu Katibu wa Kamati ya Viongozi wa Dini kwa ajili ya kuimarisha amani Zanzibar, Stanley Lichinga wa kanisa la Anglikana Zanzibar, alisema mradi huo kwa kiasi kikubwa umefanikiwa kupunguza chuki za kisiasa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ALMAS QASSIMU** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo,cha kidato cha nne chenye index namba S.1394/0098 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **KATORO ISLAMIC SEMINARY** mwaka 2012 na cheti cha chuo cha **UALIMU** kozi ya **UALIMU** chenye namba **E0573/0013** kilichotolewa na chuo cha **BUKOBA LUTHERAN TEACHERS COLLEGE(BLTC)** mwaka 2015,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa KAG/KAV/RB/662029/2020**

## KUPOTEA KWA VYETI



**MICHAEL SENKONDO** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo,cha kidato cha nne chenye index namba **S614-0074** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary LEMBENI mwaka 1999, na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S 184-0515** shule ya AGAPE LUTHERAN JUNIOR SEMINARY mwaka 2002, yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa DOD/DOD/RB/251462/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**
**SHAURI LA MIRATHI NA. 97 YA 2021**
**Maombi ya barua ya Usimamizi**
**wa Mirathi ya Marehemu**
**ELIADA MUGORE (BWIRE) MANENO-**
**…………..MAREHEMU**
**NA**
**JULIANA BWIRE…………MWOMBAJI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na Haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 10 Mwezi wa 06 mwaka 2021.
**Hati hii imetolewa tarehe 13 Mwezi wa 05 Mwaka 2021.**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya DODOMA.**
**Kituo cha DODOMA Mkoa DODOMA.**
**Usimamizi wa mirathi Na 136. /2021.**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ALLY RAMADHANI MBUYU WA DODOMA.**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA FATUMA MAFUA HASSANI**

**TANGAZO**

(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 27 mwezi 05 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 17 mwezi 05 mwaka 2021.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha KINGOLWIRA Mkoa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 15/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ABDALLAH ABDALLAH KISWILI WA MAFURU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA FARAJI BAKARI KISWILI**

**TANGAZO**

(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama ya Mwanzo)
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 26 mwezi 05 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakama kukaguliwa.
* Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
* Marehemu hakuacha wosia

**Imetolewa leo Tarehe 11 mwezi 05 Mwaka 2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaawa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 19-05-2021

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya IJUMAA tarehe 21-05-2021 Kampuni ya FAMARI INVESTMENT itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA gari hilo lenye namba za usajili

   **T 428 DPN / T 848 DPC**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 21 |
| Upana | - | mita | 3.2 |
| Kimo | - | mita | 5.0 |

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM** hadi **TUNDUMA** kupitia **VIGWAZA/MAKAMBAKO & MPEMBA**

Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaawa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 19-05-2021

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **IJUMAA** tarehe 21-05-2021 Kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea TUNDUMA gari hilo lenye namba za usajili

   **T 592 DQU / T 281 DBY**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 21 |
| Upana | - | mita | 3.1 |
| Kimo | - | mita | 5.2 |

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM** hadi **TUNDUMA** kupitia **VIGWAZA/MAKAMBAKO & MPEMBA**

Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**AMANI YUSUPH KIJINGA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 426 BYP – BOXER BAJAJ. CHASSIS NAMBA **MD2A21BY4JWA91941.** ENGINE NAMBA **PFZWJM68275.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/URA/RB/251012/2021.**




**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# DC Liwale ahadharisha wakulima kuhusu tembo

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Sarah Chiwamba, amewataka wakulima kuacha maeneo ambayo ni mapito ya asili yanayotumiwa na tembo ili kuepuka kushambuliwa na wanyama hao.

Sarah alisema hayo, juzi wakati akizungumza na wakazi wa vijiji vya Ngumbu, Barikiwa, Mtawatawa, Mkutano na Lilombe, Kata ya Kibutuka, alipokwenda kukagua uharibifu uliosababishwa na tembo hao katika mashamba yao.

Pia alisema, halmashauri inafanya mchakato kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi kijiji hicho, huku wataalamu wakiendelea kutoa ya kutunza misitu yao ya vijiji badala ya kulima katika maeneo ya misitu.

"Vilevile, ninawataka muache mara moja kulima maeneo ambayo ni mapito ya asili ya wanyama hao na halmashauri iko kwenye mchakato wa kuhakikisha inafanyia matumizi bora ya ardhi ya vijiji vyenu," alisema Sarah.

Alisema, katika uvamizi wa tembo hao uliofanyika wiki iliyopita, hakuna mauaji kwa binadamu na kwamba baadhi ya mashamba ya wananchi yameharibiwa hasa ya mazao ya chakula kama mtama, mbaazi na mihogo.

"Hata mashamba ya ufuta na mikorosho yameharibiwa kwa kuvunjwa matawi na pia ufuta kukanyagwa, kwani kwa kawaida tembo huwa hawali mazao hayo ila wanafanya uharibifu tu," alisema.

Aidha, alisema Serikali inaendelea na tathmini kuona uharibifu uliotokea ili taratibu zingine za kisheria za kuwalipa kifuta jasho zifanyike na kuwataka waendelee kuwa watulivu.

Ofisa Maliasili wa wilaya huyo, Damas Mumwi, alisema, eneo hilo linalotumiwa kwa kilimo, ni mapito ya tembo ya miaka mingi, hivyo ni vyema likaachwa ili wanyama hao waendelee kulitumia kama njia.



Mkuu wa Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Sarah Chiwamba (katikati), akiwa katika ziara ya kukagua mashamba ya wakulima, kujionea uharibifu wa mazao uliosababishwa na tembo, katika Kijiji cha Ngumbu, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uzalishaji maziwa kupaa

**Na Enock Charles**

UZALISHAJI wa maziwa katika mikoa minne nchini umepangwa kuongeza lita milioni 23 kufikia mwaka 2024 kupitia mradi wa maziwa wa AgResults, ulioanzisha shindano la uhamasishaji wa ufugaji bora na wenye tija ikiwamo uhimilishaji na matumizi ya pembejeo zenye ubora litakalohusisha wafanyabiashara wa pembejeo za mifugo.

Kiongozi wa mradi huo, Neema Mrema, alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari wakati wa mafunzo kwa washindani wa mradi huo kuwa ufagaji wanaotaka kuuhamasisha ni utakaoleta tija kubwa kwa wafugaji na jamii inayowazunguka tofauti na ufugaji wa kienyeji ambao hauna manufaa makubwa kwa wafugaji hao.

"Mradi huu una malengo makuu matatu, kwanza kabisa ni kuongeza uzalishaji wa maziwa kwa wafugaji wadogo wenye ng'ombe 1-10, kuongeza tija kwenye uzalishaji wa maziwa na kuboresha soko kwa wafugaji," alisema Neema.

Mradi huo unaoanza mwaka huu unahusisha wauza pembejeo za mifugo walioko kwenye eneo la mradi unaogusa mikoa minne ambayo ni Dar es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024.

**"Mradi huu una malengo makuu matatu, kwanza kabisa ni kuongeza uzalishaji wa maziwa kwa wafugaji wadogo wenye ng'ombe 1-10, kuongeza tija kwenye uzalishaji wa maziwa na kuboresha soko kwa wafugaji," alisema Neema.**

# Wajawazito wahimizwa kupima uzito

**Na Joseph Mwendapole**

WAJAWAZITO wamekumbushwa kupima uzito mara kwa mara kwa ajili ya maendeleo ya ukuaji wa mtoto aliyetumboni na kwa afya yao.

Ushauri huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya Vijibweni Kigamboni jijini Dar es Salaam, Thomas Bwire.

Alikuwa akizungumza wakati wa ziara ya Wakala wa Vipimo (WMA), kwa ajili ya kupima mizani ya hospitali hiyo kama sehemu ya madhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani inayoadhimishwa Mei 20 kila mwaka. Katika kuadhimisha Siku ya Vipimo Duniani (WMA), inahakiki mizani katika zahanati, vituo vya afya na hospitali zote nchini.

Dk. Bwire alisema ni muhimu wanawake wajawazito kujitokeza kupima kwani kunawasaidia madaktari na wahudumu wa afya kujua uzito wao hivyo kuwashuari vyema namna ya kuenenda hadi siku ya kujifungua.

Alisema wamekuwa wakihakiki mizani yao mara kwa mara kwa sababu vipimo sahihi ni muhimu kwa ajili ya tiba sahihi kwa watoto, wajawazito na wagonjwa kwa ujumla.

"Dawa zinatolewa kulingana na uzito wa mtu sasa kama hujui uzito sahihi wa mgonjwa unaweza kumzidishia dawa ukamsababishia matatizo kwa hiyo lazima tuwe na vipimo sahihi kwa ajili ya tiba sahihi," alisema.

Kaimu Meneja wa WMA Temeke mkoani Dar es Salaam, Krishna Mganyizi, alisema wamekuwa wakifanya uhakiki wa vipimo mara kwa mara ili kuhakikisha vipimo vinavyofanyika vinakuwa sahihi.



# LIVERPOOL, CITY ZAMWANIA MARTINEZ

**MANCHESTER, England**

LAUTARO Martinez huenda akawa mrithi wa Sergio Aguero katika klabu ya Manchester City pale Etihad.

Kwa mujibu wa 90min.com City na Liverpool zimekaa tayari kuwania saini ya mshambuliaji huyo wa Inter Milan kipindi cha majira ya joto.

Ingawa Inter imeweka dau la pauni milioni 100, lakini wamedai wanaweza kushusha mpaka angalau mpaka pauni milioni 70.


Raia huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 23 amekuwa akiwaniwa na timu hizo za Ligi Kuu England kutokana ubora alioonyesha akiwa na Romelo Lukaku pale Inter msimu huu.

Martinez amecheza mechi 36 na Inter huku akiwa amefunga mabao 16 na kutoa pasi za mwisho nane.

City wanahitaji saini ya mshambuliaji huyo ili awe mrithi wa Aguero ambaye atatimka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu.

Itakumbukwa kuwa Lionel Messi aliwahi kumtaja Lautaro kama mshambuliaji aliyekamilika.

Endapo atafanikiwa kusainiwa katika klabu yoyote kati ya hizi, basi kijana huyu mwenye umri mdogo kabisa anaweza kujitengenezea ufalme na kuendeleza ubora wake.



# JORGINHO ATAKIWA CHELSEA

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imeingia kwenye rada za kutaka kunyakua saini ya mchezaji wa Chelsea, Jorginho kwa mabadilishano na kiungo wao Miralem Pjanic endapo Blues hao watahitaji huduma ya mchezaji huyo.

Jorginho amekuwa na kipindi kizuri katika timu ya Chelsea, lakini kocha wa timu hiyo Thomas Tuchel ana mipango mikubwa msimu ujao ikiwamo kumsajili Pjanic ili kuongeza nguvu kwenye safu yake ya ushambuliaji.

Barcelona wanategemea kuendelea kubaki na Pjanic kutokana na uwezekano wa kutosajili wapya mwisho wa msimu huu.

Na kigezo pekee cha kumwachia mchezaji huyo ni kubadilishana na Jorginho, ambaye amekuwa akifanya vyema sana toka ujio wa Tuchel pale darajani.

Tuchel amekuwa mpenzi mkubwa wa Pjanic toka alivyokuwa PSG na anaamini anaweza kuwa ingizo bora na muhimu sana kwenye timu ya Chelsea ambayo ina malengo makubwa sana msimu ujao.

Pjanic hajawa na msimu mzuri sana pale Camp Nou msimu huu, huku akiwa amecheza michezo 28 na hajafanikiwa kufunga goli wala kutoa pasi ya magoli. Pia, hajacheza mchezo wowote wa La Liga toka mwezi Februari, mwaka huu.

# CAVANI AFUNGUKA KILICHOMBAKISHA UNITED

**MANCHESTER, England**

EDINSON Cavani amesema mazingira mazuri ya Manchester United yamechangia yeye kuamua kubakia hapo Old Trafford.

Cavani ameongeza mkataba wa mwaka mmoja kubakia hapo United baada ya awali kuripotiwa anataka kuondoka.

Katika mazungumzo na kipindi maalumu cha televisheni ya United, Cavani alieleza kuwa kiwango kikubwa wachezaji wenzake wamechangia yeye kusalia klabuni hapo.

Cavani ameonyesha furaha yake kwa viongozi, wachezaji, mashabiki na kila mdau wa United kwa kumwamini.

Alisema kuna wakati wachezaji wenzake walimwambia asiondoke bado wanamhitaji na wanatamani aendelee kusalia hapo na bila hiyana yeye akaamua kukubali.

Vilevile imani kubwa aliyoonyesha kocha wake, Ole Gunaer Solskjaer imemwongezea kujiamini na anaweza kuwa na wakati mzuri pale Old Trafford.



## HABARI MICHEZO




# GREENWOOD

## ALITAKA TAJI EUROPA

**MANCHESTER, England**

NYOTA Mason Greenwood anazingatia baraka za Manchester United kutwaa taji la Ligi ya Europa wakati kiwango chake msimu huu kikiendelea kukua.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 alifurahia msimu huu hapo Old Trafford wakati msimu uliopita, akifunga mabao 17 yakifanya kuwa mchezaji kinda zaidi katika historia ya United.

Tangu Aprili Mosi, Greenwood alikuwa na mabao nane katika michezo 11, na sita kati ya michezo saba kwenye Ligi Kuu England.

Utulivu wote utahamia fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Villarreal kule Gdansk, wakati Mashetani Wekundu watataka kushinda heshima kubwa ya kwanza tangu kuinua kombe hilo miaka minne iliyopita.

"Kushinda kitu na United itakuwa jambo zuri sana," alisema Greenwood akiiambia Sky Sports.

"Nataka kufanya hivyo. Tuko katika nafasi nzuri ya kuifanya kumaliza vizuri msimu wa Ligi Kuu England na kushinda katika fainali itakuwa nzuri. Tunahitaji taji, hatujapata lolote kwa miaka ya hivi karibuni."

## MOUNT ACHAGULIWA CHELSEA

**LONDON, England**

MCHEZAJI wa Chelsea, Mason Mount amechaguliwa mchezaji bora wa timu hiyo kwa msimu wa 2020/2021.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 22, ameonyesha makali yote licha ya mabadiliko ya walimu ambayo yametokea pale Stamford Bridge.

Akiwa chini ya Frank Lampard, Mount alikuwa wa moto sana katika eneo la katikati, kushambulia licha ya kujali atatokea kati au pembeni.

Mount amekuwa mwiba wa moto kwa wapinzani pindi anapokuwa uwanjani na amesaidia timu yake ya Chelsea kufanya makubwa sana na mpaka sasa kuwa kwenye fainali ya Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya ambayo itapigwa mwishoni mwa mwezi huu dhidi ya mabingwa wa EPL, Manchester City.

Mount anakuwa mchezaji wa kwanza kushinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka kutokea kwenye akademi ya timu hiyo toka tukio hilo lifanywe na John Terry mwaka 2006.

Huu waweza kuwa mwanzo mzuri kwa kinda huyu ambaye anaonekana kuja kwa kasi sana chini ya Tuchel ambaye ameibadilili Chelsea kwa kiwango kikubwa sana toka ujio wake pale Darajani. Akiwa na Chelsea msimu huu amecheza mechi 34 na kufunga magoli sita huku akitoa pasi za magoli sita pia, ila anapokuwa uwanjani basi huwa anawaonea sana wapinzani.

# GUARDIOLA AMPA JUKUMU AGUERO



**MANCHESTER, England**

KOCHA Mkuu wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema kuwa anataka kumuona mshambuliaji wake Sergio Aguero anaonyesha kiwango cha juu uwanjani na anahitaji kumwona akicheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kiwango cha nyota huyo ndani ya kikosi cha City kimezidi kuporomoka kwa sasa jambo ambalo limekuwa likimfanya akose kujiamini.

Pia kwa sasa imekuwa ikielezwa kuwa Guardiola hana uhusiano mzuri na Aguero jambo ambalo limekuwa likimfanya awe anamweka benchi.

Aguero msimu utakapomeguka atasepa mazima kwa kuwa mkataba wake unakwisha na timu ilitoa taarifa rasmi kwamba haitamwongeza mkataba mwingine.

Guardiola amesema: "Nafikiri kwenye mchezo dhidi ya Newcastle alikuwa hayupo fiti lakini hata sasa bado hajawa fiti asilimia 100, nafikiri atakuwa tayari kwa michezo kadhaa.

"Bado kuna michezo kadhaa na ninadhani nitafanya uamuzi mgumu katika mchezo wa fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mbele ya Chelsea nafikiri anaweza kucheza."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# CHELSEA YATANGAZA KUMWANIA LEWANDOWSKI

Katika vita ya kumwania mshambuliaji huyo itachuana na PSG, Barcelona...

**LONDON, England**

CHELSEA imeripotiwa inafanya majadiliano na mabingwa wa Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga, Bayern Munich ili kumsajili mshambuliaji wake tegemeo, Robert Lewandowski, kwa mujibu wa Sky Sport Ujerumani.

Lewandowski anaweza kuongeza mkataba na Bayern Munich hadi mwaka 2023, lakini bado kuna sintofahamu kuhusu majaliwa yake.

Paris Saint-Germain imekuwa ikihusishwa na mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Poland, hasa kama miamba hao wa jiji la Paris wataachana na Mfaransa Kylian Mbappe.

Wakala wa mchezaji huyo ameripotiwa akiipa presha Bayern ili wafikie muafaka na mteja wake kabla ya mwisho wa msimu huu.

Kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel amebainisha kwamba, anamtaka Lewandowski katika kuimarisha kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao.

Hata hivyo, Tuchel atakabiliwa na ushindani mkubwa wa kuwania saini ya nyota huyo kutoka kwa Paris Saint-Germain na Barcelona.

Lewandowski ameripotiwa kuwa hana mpango wa kuongeza mkataba na Bayern ambako alijiunga nao tangu mwaka 2014.

## KWA UFUPI

**KANE AITAMANI CITY**
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya England, Harry Kane, anataka kuhamia katika klabu ya Manchester City kwa dau la pauni milioni 100 mwishoni mwa msimu huu.

**KANE MTEGONI UNITED**
KLABU ya Manchester United inamchunguza mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27 licha ya kwamba, Spurs haiko tayari kumuuza. ***(Mirror)***

**SPURS, KANE ZILIJIPANGA**
KLABU ya Tottenham Hotspur ilianza mipango ya kumuuza Harry Kane Februari mwaka huu. Nyota huyo tayari amebainisha wazi anataka kuondoka mwishoni mwa msimu huu. ***(Mail)***

**LAMPARD ANUKIA PALACE**
KLABU ya Crystal Palace ipo katika mazungumzo na aliyekuwa kocha wa Chelsea na kiungo wa kati wa England, Frank Lampard mwenye umri wa miaka 42, kuhusu kumrithi Roy Hodgson. ***(Talksport)***

**HOWE KUMRITHI HODGSON**
ALIYEKUWA kocha wa Bounemouth, Eddie Howe mwenye umri wa miaka 43 yupo katika orodha ya kumrithi Roy Hodgson mwenye umri wa miaka 73.

**COOPER, ISMAEL WACHUANA**
KOCHA wa Swansea mwenye umri wa miaka 42, Steve Cooper na kocha wa Barnsley, Valerien Ismael mwenye miaka 45 pia wanaonekana kuwa mbele kuchukua nafasi ya Roy Hodgson. ***(Sky Sports)***

**WILLIAN KWENDA MAREKANI**
WINGA wa Arsenal na Brazil mwenye umri wa miaka 32, Willian anataka kuondoka ili kujiunga na klabu ya David Beckham, Inter ya Miami Marekani. ***(Sun)***

**NETO ATAJWA ARSENAL**
BARCELONA inaweza kumwachia golikipa wa Brazil, Neto mwishoni mwa msimu huu huku Arsenal ikiwa na hamu ya kuendelea kusaka saini ya kipa huyo mwenye umri wa miaka 31. ***(Mundo Deportivo)***

**DELANEY SOKONI EPL**
KLABU ya Southampton inapanga kuwasilisha ombi la kumnunua kiungo wa kati wa Denmark na Borussia Dortmund, Thomas Delaney mwenye umri wa miaka 29. ***(ESPN)***

**GINTER AGOMBEWA ULAYA**
KLABU ya Tottenham imewasilisha ombi la kutaka kumsajili beki wa Borussia Monchengladbach na Ujerumani, Matthias Ginter, lakini inakabiliwa ushindani kutoka kwa Liverpool na Inter Milan. ***(Bild)***

**VILLA YAMFUATA ZERKANE**
ASTON Villa imewasiliana na wawakilishi wa winga wa Algeria na Bordeaux, Mehdi Zerkane mwenye umri wa miaka 21. ***(L'Equipe)***



HABARI MICHEZO

# AZAM, BIASHARA UNITED MECHI YA VIWANGO BARA

**Na Saada Akida**

VITA ya kuwania pointi tatu muhimu inatarajia kuendelea tena kwa 'Wauza Lambalamba' Azam FC kuwakaribisha Biashara United kutoka Musoma mkoani Mara katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Azam FC ambayo imerejea katika makali yake, itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kuichapa KMC FC mabao 2-1, ikiwa ni kulipa kisasi cha kufungwa bao 1-0 katika mchezo wa mzunguko wa kwanza.

**Akizungumza na gazeti hili jijini, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, alisema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mechi hiyo na wamejipanga kuingia dimbani kusaka pointi tatu muhimu na kujiweka katika mazingira mazuri katika msimamo wa ligi hiyo.**

Vivier alisema wanahitaji kuwakaribia vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga ambao wako katika nafasi za juu.

Alisema kuelekea mchezo huo hakuna majeruhi na suala la nani atacheza litabaki kuwa huru na Kocha Mkuu, George Lwandamina atapanga kikosi chake kwa amani.

"Biashara United ni timu nzuri na wako vizuri, tumeshafanyia kazi ubora na mapungufu yao na tayari wameshafanyia kazi na wako tayari kwa ajili ya kutafuta pointi tatu muhimu."

"Malengo yetu ni kuhakikisha tunatafuta pointi tatu muhimu ili kujiweka katika nafasi nzuri katika mbio za kupambana na walikuwa juu yetu," alisema Vivier.

Azam FC iko katika nafasi ya tatu imekusanya pointi 57 na kucheza mechi 29, inakutana na Biashara United iliyo kwenye nafasi ya nne na wamejikusanyia pointi 45 baada ya kushuka dimbani mara 29.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Highland Estates itakuwa ni kati ya wenyeji Ihefu



Golikipa wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Janeth Shija (kulia), akifanya mazoezi chini ya uangalizi wa kocha wa makipa wa timu hiyo, Fatuma Omary kwa ajili ya kujiandaa na mechi za kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika. PICHA: TFF

# Badru aanza na neema Mtibwa

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa Mtibwa Sugar, Mohamed Badru, ameanza na mguu mzuri baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro juzi.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kumalizika, Badru ambaye kabla alikuwa akiifundisha Gwambina FC, alionyesha kufurahishwa na ushindi huo na kusema ilikuwa ni mikakati maalumu, licha ya kuifundisha timu hiyo kwa siku mbili tu.

Badru alisema ametua Mtibwa Sugar kwa lengo moja la kuinusuru timu hiyo na anaamini watafikia ndoto hizo.

"Mchezo ulikuwa mzuri. Kila timu ilimheshimu mwenzake, hasa mimi. Nilicheza kwa kujilinda na kushambulia kwa kushtukiza kwa sababu tulihitaji zaidi ushindi na nashukuru wachezaji wangu walifanya kile ambacho nilikuwa nahitaji," alisema Badru.

Kocha huyo alisema amefurahishwa na aina ya wachezaji ambao amewakuta Mtibwa Sugar akiongeza wana uzoefu tofauti na timu yake ya zamani .

"Nilipofika Mtibwa Sugar nimekutana na wachezaji wazoefu, wakongwe na wenye uwezo mkubwa wa kuuchezea mpira, hii inanifanya niamini kabisa kwa kushirikiana nao pamoja, tutaibakisha timu hii katika Ligi Kuu," alisema kocha huyo. Badru amerithi mikoba ya Vicent Barnabas ambaye alikuwa akikaimu nafasi iliyoachwa na Thierry Hitimana.

## NYOTA POLISI TZ WAPEWA LIKIZO

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Polisi Tanzania umewapa mapumziko ya siku nane wachezaji wake na watarejea tena kambini ifikapo Mei 25, mwaka huu kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya mechi zilizobakia za Ligi Kuu Bara, imefahamika.

Ofisa Habari wa timu hiyo, Frank Lukwaro alisema mapumziko hayo yametoka na kikosi chao kutokuwa na mchezo wa mashindano ya Kombe la FA, hivyo benchi la ufundi limeamua kutoa ruhusa hiyo ya kwenda kusalimia familia zao.

Lukwaro alisema anaamini mapumziko hayo yatasaidia kuwajenga wachezaji wao na watakaporejea watakuwa na nguvu mpya ya kuendeleza mapambano.

Aliongeza baada ya kurejea ataandaa programu maalumu itakayowarejesha mchezoni nyota wake na hatimaye kumaliza msimu kwa kupata matokeo chanya.

"Tunatarajia kucheza mechi moja ya kirafiki kwa ajili ya kujiwinda na mchezo wetu dhidi ya Simba na ile iliyosalia ya Ligi Kuu Bara msimu huu," alisema Lukwaro.

Polisi Tanzania imebakiza michezo minne ili kumaliza msimu ambayo ni dhidi ya Simba, Kagera Sugar, Mwadui FC na Ruvu Shooting.

## ALLIANCE GIRLS KUSAJILI SABA

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Alliance Girls ya jijini Mwanza inatarajia kusajili wachezaji wapya saba kwa ajili ya kujiimarisha na msimu ujao wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Alliance Girls, Ezekiel Chobanka alisema wamejiandaa kuongeza nguvu katika kikosi chao na wachezaji watakaowasajili watatoka ndani na nje ya Tanzania.

"Nina mpango wa kusajili wachezaji kutoka Kenya, nafahamu majirani zetu Kenya ni sehemu mojawapo kati ya nchi zenye kuzalisha wachezaji wazuri wanawake, na wengine baadhi nitawachukua kutoka kwenye klabu zetu za hapa nyumbani," alisema Ezekiel.

Kocha huyo alisema tayari ameshakabidhi ripoti ya ufundi kwa uongozi wa timu hiyo ambao tayari wameonyesha nia ya kuyafanyia kazi mapendekezo yake ili kupata kikosi chenye ushindani kwa ajili ya msimu mpya.

Alliance Girls imemaliza msimu huu ikiwa katika nafasi ya sita baada ya kujikusanyia pointi 27 wakati mabingwa ni Simba Queens wakifuatiwa na watani zao, Yanga Princess.

Michezo
Alhamisi Mei 20, 2021
Nipashe



CHELSEA YATANGAZA KUMWANIA LEWANDOWSKI

HABARI UK 22




Kiungo wa Yanga, Tuisila Kisinda (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa JKT Tanzania, David Mwantika katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## YANGA YAIKAMATA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

MABAO ya kipindi cha kwanza yaliyofungwa na Yacouba Songne na Mkongomani Tuisila Kisinda yaliifanya Yanga kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Dodoma Jiji katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana.

Ushindi huo umeifanya Yanga kufikisha pointi 61 sawa na vinara wa Ligi Kuu Bara, Simba lakini ikibaki kwenye nafasi ya pili kwa sababu mabingwa hao watetezi wana idadi nzuri ya mabao ya kufunga.

Yacouba aliipatia Yanga bao la kwanza dakika ya 26 kwa kichwa baada ya kuitendea haki krosi iliyopigwa na beki wa kulia, Kibwana Shomari.

Alikuwa ni Mkongomani Kisinda aliyefunga bao la pili dakika tatu baadaye akitumia makosa ya mabeki watatu wa JKT Tanzania ambao wote walishindwa kuzuia krosi ya Ditram Nchimbi ambayo ilimkuta mfungaji akiwa peke yake na kuujaza wavuni kirahisi.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko, Yanga ikiwatoa Saido Ntibazonkiza, Nchimbi na Tuisila, nafasi zao kuchukuliwa na Deus Kaseke, Zawadi Mauya na Waziri Junior, huku JKT Tanzania ikiwatoa Shaaban Mgandila, Kigi Makasi na Rashid Mandawa, nafasi zao kuchukuliwa na Kelvin Nashon, Hassan Twalib na Mussa Said, lakini hayakubadilisha matokeo ya kipindi cha kwanza.

JKT Tanzania iliyocheza mechi 30 iko katika nafasi ya 14 kwenye msimamo wa ligi hiyo yenye timu 18 ikiwa na pointi 33 na ikibakisha michezo minne ili kumaliza msimu huu 2020/21.

# AMA ZAO AMA ZETU

### ●●●Serikali yaitakia heri Simba kuelekea mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika...

**Saada Akida na Augusta Njoji, DODOMA**

WAKATI uongozi wa Simba ukisema wanaimani na matarajio ya timu yao kupata ushindi wa mabao 5-0 katika mechi ya marudiano ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Kaizer Chiefs na kusonga mbele, serikali imewatakia heri wawakilishi hao wa nchi.

Simba ambayo ililala mabao 4-0 katika mchezo wa kwanza ugenini Johannesburg, Afrika Kusini, kesho itawakaribisha Kaizer Chiefs kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na jijini jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara alisema wanafahamu wana 'mzigo mkubwa' wa kupata matokeo ya mabao 5-0, lakini wana imani wachezaji wakijitoa kwa asilimia 100 watafanya vizuri na kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo.

Manara alisema endapo wachezaji watafuata maelekezo ya benchi la ufundi, watafanikiwa 'kupindua' matokeo yaliyopatikana Afrika Kusini na kurudisha historia ya miaka 42 iliyopita ambayo ilifanywa na nyota waliotangulia wa timu hiyo kwa kuwafunga Mufulila Wanderers.

"Mechi yetu ya kwanza hatukucheza vizuri kama tulivyoizoea Simba, nina imani wachezaji wa Simba wakijitoa kwa asilimia 100 , wanatakiwa kupigana kwa jasho na damu, tutashinda mechi hiyo, kama wasipojitoa kwa asilimia hizo basi hatuwezi kucheza nusu fainali."

"Sijawahi kulala kambini, ila kutokana na ugumu na umuhimu wa mchezo huu nitaiacha nyumba yangu na kwenda kulala kambini kwa ajili ya kuwatia moyo wachezaji ili kuhakikisha tunafanya vizuri kwenye mechi hiyo," alisema Manara.

Alimtaja mgeni rasmi katika mechi hiyo atakuwa Mkuu wa Mkoa mpya wa Dar es Salaam, Amos Makala.

Aliitaja kauli mbiu ya mchezo huo ambao ni muhimu sana katika timu yao ni "Ama zetu, ama zao", "Do or Die Sessions Two".

Aliongeza Simba kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imeliandikia Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kuomba kuongezewa idadi ya mashabiki watakaoingia uwanjani kutoka 10,000 hadi kufikia mashabiki 30,000.

"Bado hatujapata taarifa rasmi kuhusu ujio wa wapinzani wetu, ila tunajua wanakuja lini na wapi wanafikia na mmoja wa viongozi wa wapinzani wetu (Yanga), anawasaidia Kaizer Chief, ila hilo hatujali."

"Mashabiki wanatakiwa kujitokeza kwa wingi wakivalia jezi nyeupe na nyekundu, ila wale walionunua jezi za wapinzani wetu tunawaruhusu kuja ila nina imani mwisho wa siku wataondoka uwanjani kwa aibu," alisema Manara.

Mapema jana asubuhi, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa akiwa bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Makete (CCM), Festo Sanga aliwataka Watanzania kuungana kuelekea mchezo huo wa kimataifa.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema Mei 22, mwaka huu kutakuwa na mchezo mkubwa ambao unaweza kubeba rekodi ya nchi na utaenda kubeba mafanikio ya timu takribani nne endapo Simba itafuzu kucheza nusu fainali ikiwamo Yanga na timu nyingine.

"Je, ni mkakati upi wa serikali kuhakikisha Simba Sports Club inashinda na mashabiki wanajaa uwanjani," alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri Bashungwa alisema timu inaposhinda na kuwakilisha nchi inakuwa ni timu ya Taifa.

"Nitumie nafasi hii kuipongeza Simba Sports Club kwa hatua waliyofikia, nitoe wito kwa Watanzania wote kuhakikisha tunaiunga mkono ili mechi itakayochezwa tarehe 22 wapate ushindi kwa kuwa ushindi huo utaleta heshima ndani ya nchi yetu."

"Tunawatakia heri Simba na sisi seri-

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002